Haliuzwi
FEBRUARI 3, 2026
/islamicftz
Shaban 15 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 569
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah


## Rais Samia azuru UAE kushiriki World Government Summit



# Nahdi, Sheikh Barahiyan wahimiza matumizi zaidi ya 'media' kueneza da'awah

- Watajwa chachu ya maendeleo ya Uislamu






## Wahitimu 70 waagwa Maahad Imam Shafii kwa nasaha nzito

## Mwinyi ahimiza umuhimu kujipamba na Qurani, malezi bora kwa vijana




## Hisa za makampuni mawili tu zakidhi vigezo halal DSE

## Sheikh Ibrahim Twaha aonya michezo, pumbao ndani ya Ramadhan



## Serikali yaonya wanaopandisha bei za bidhaa kuelekea Ramadhan

HABARI TANGA

NA YUSUPH AMIN




# Sheikh Ibrahim Twaha aonya michezo, pumbao ndani ya Ramadhan

Mlinganiaji na Mhubiri wa Dini ya Kiislamu nchini, Sheikh Ibrahim Twaha, amesema moja ya mbinu anazozitumia Iblis (shetani aliyelaaniwa) katika kuwahadaa Waislamu wasifikie kilele cha ubora wa funga ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan ni kuwashughulisha na mambo ya pumbao ukiwamo mchezo wa soka.

Amesema wakati Waislamu wakiendelea na maandalizi ya kuupokea mwezi wa Ramadhan, shetani naye anajiandaa kuwapotosha waja juu ya taratibu za kuupokea mwezi huo Mtukufu.

Sheikh Twaha si Mlinganiaji wa kwanza kuzungumzia kadhia hii katika siku za karibuni; wapo Masheikh wengine waliokemea kwa uwazi jambo hili akiwamo Sheikh Abdulbasit Othman na Sheikh Hashim Rusaganya.

Katika khutba yake ya ibada ya sala ya Ijumaa, aliyoitoa katika Masjid Ansaar, barabara ya 19 jijini Tanga, Sheikh Ibrahim Twaha aliutaja mchezo wa soka, karata na dhumna kama silaha kubwa ambazo Iblis huzitumia ili kuwapoteza Waislamu wasinufaike na matunda ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Ameeleza kuwa waja wema waliopita hawakuikaribisha Ramadhan kwa kununua karata wala dhumna, bali walikuwa wanaachana na kazi zote katika mwezi wa Ramadhan na kumuelekea Allah Ta'ala kwa ibada.

Miongoni mwa waja wema aliowatolea mfano ni Imam Ahmad bin Hanbal (Allah amrehemu) ambaye alikuwa anaacha darsa za kawaida na kufundisha darsa zinazohusiana na mwezi wa Shaaban kwa ajili ya kujiandaa na mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

"Shetani ndiye ambaye anawaelekeza mnunue karata na kuzicheza ndani ya Ramadhan. Zaidi ya hivyo, sasa hivi watu wengi hawamchi Allah na wanafuata mienendo ya shetani," alisema Sheikh Twaha ambaye pia ni Mkurugenzi wa taasisi ya The Islamic Foundation.

Katika khutba yake, Sheikh Twaha amesema hali ni mbaya zaidi katika kipindi hiki, ambapo maadui wa Uislamu kwa kushirikiana na shetani wamekuwa wakiandaa ligi mbalimbali wakizinasibisha na Ramadhan.

Amesema moja ya mbinu wanazotumia katika kuwapoteza Waislamu ni kupanga baadhi ya mechi nyakati za usiku, na katika hilo wapo baadhi ya Waislamu ambao wanaacha kusali Sunna ya Tarawehe na Tahajjud kwa sababu ya kufuatilia mechi hizo.

"Mpira utakusaidia nini mbele ya Allah Ta'ala..., kutengeneza logo za Ramadhan kutakusaidia nini mbele ya Allah Ta'ala. Na ukisema unacheza mpira huku unafanya ibada, ni aibu kwako ewe mja wa Allah. Jiulize, hizo ndizo kazi za Ramadhan?" alihoji Sheikh Twaha huku akinukuu hadith ya Mtume (rehema za Allah na amani ziwe juu yake) inayosema: "Amepata hasara yule ambaye ameidiriki Ramadhan kisha hakusamehewa (madhambi yake)."

Mbinu ya pili aliyoitaja Sheikh Twaha ni Iblis kuwafanya Waislamu wahisi uzito katika kumuadudu Allah na kuona funga ya Ramadhan ni ibada ngumu. Amesema hiyo ni moja ya kazi na vitimbi vya shetani katika kuwaelekeza watu jinsi ya kuupokea mwezi wa Ramadhan.

Sheikh Twaha ametanabahisha kuwa wapo Waislamu wanaoona ni bora wasimtii Allah katika mwezi wa Shaaban na badala yake waendelee kumuasi Allah kidogo kidogo ndani ya mwezi huu na watakuja kufanya ibada katika mwezi wa Ramadhan.

Sheikh Twaha alihoji: "Ni watu wangapi mpaka sasa hivi wameshaenda kuchukua vipimo mbalimbali na uthibitisho mbalimbali eti wanaumwa vidonda vya tumbo wakidai kuwa ni ngumu kupona, Enyi Waislamu, hivi mnamdanganya nani. Unawadanganya viumbe, au unamdanganya Allah. Katu huwezi kumdanganya Allah Subhanahu Wata'ala."

"Na ikiwa unamdngaanya kiumbe, kwani yeye ndiye mwenye malipo? Atakulipa kwenye ibada zako? Atakunusuru na Moto wa Jehannam? Atakunusuru na adhabu za kaburi? Atakusaidia kujibu maswali ya kaburini?" alionya Sheikh Twaha na kuwasihi wale wote wanaoacha kufunga swaumu ya Ramadhan kwa dharura zisizo na mashiko kisheria kuacha visingizio.

Ameongeza kuwa katika dunia hii binadamu si lolote si chochote, bali Allah ndiyo kimbilio, ndiye anayestahiki kuogopwa na kumshtakia kwa kila jambo. Katika hali ya kustaajabisha, Sheikh Twaha amesema wapo baadhi ya watu ambao maandalizi yao mpaka muda huu yanaenda sambamba na maandalizi ya shetani katika kuupotosha umma na kuutia uzito katika kufanya ibada pamoja na kuupokea mwezi wa Ramadhan.

"Wema waliotangulia walikuwa wakimuomba Allah awafikishe Ramadhan miezi sita kabla, na baada ya Ramadhan walikuwa wakimuomba Allah awakubalie matendo yao waliyoyafanya ndani ya Ramadhan," alisema na kusisitiza kuwa Muislamu wa kweli hawezi katu kukubali kufuata vitimbi na muongozo wa shetani katika kumzuia kutekeleza ibada za Mwenyezi Mungu.

Kwa kuzingatia hilo, Sheikh Twaha amewasihi Waislamu kudumu katika ibada na kumuepuka shetani: "Usimtii shetani akakuaminisha kuwa ibada katika mwezi wa Ramadhan ni nzito. Watu wangapi wanaiacha miji yao na kuelekea katika nchi nyingine ilimradi tu wajihalalishie kutofunga Ramadhan. Anaona aibu kubaki katika mkoa wake kwa sababu watu watamuona hafungi. Muogope Allah ewe Muislamu na ufanye matendo ambayo hautajali kama mtu atajua au hatajua isipokuwa Allah."

Aidha, Sheikh Twaha alifahamisha kuwa kila inapokaribia Ramadhan shetani huwagombanisha watu, na inafikia wakati mtu anagombana na mkewe pasina sababu yoyote, ndugu hawasalimiani, hawatembeleani wala kujuliana hali, ilimradi tu waingie katika Ramadhan hali ya kuwa wamegombana.

Sheikh Twaha alitaja mbinu ya tatu anayoitumia Iblis kuwa ni kuwajengea watu mazingira ya kuchukua mikopo ya riba katika mwezi wa Shaban ili wale vizuri katika mwezi wa Ramadhan. Juu ya hilo, Sheikh Twaha aliitaja hadithi ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) isemayo: "Hakika Mwenyezi Mungu ni Mzuri, hakubali ila kilicho kizuri." [Muslim].

Kwa kuzingatia mafundisho haya ya Mtume, Sheikh Twaha amewatoa wasiwasi Waislamu kwamba iwapo watamtegemea Allah kikweli kweli atawapa riziki nzuri, kwani hata Masahaba wa Mtume (Allah awaridhie) waliishi kwa shida na walikuwa hawajui watafuturu nini ndani ya Ramadhan, lakini kwa uwezo wake Allah walipata chakula na kuweza kufunga kikamilifu.

شَعْبان

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

## Sheikh Ibrahim Twaha aonya michezo, pumbao ndani ya Ramadhan









NA BIN HAJJ IBRAHIMU HAJJ

# Nahdi, Sheikh Barahiyan wahimiza matumizi zaidi ya 'media' kueneza da'awah

Mudir wa Taasisi ya Ansaar Muslim Youth Centre (AMYC), Sheikh Salim Barahiyan, pamoja na Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, wametoa wito kwa masheikh na Waislamu kwa ujumla kuwekeza zaidi katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kama njia ya kufikisha mafundisho sahihi ya Uislamu na kuinusuru jamii dhidi ya upotoshaji unaosambazwa na watu wa baatili.

Wawili hao walitoa kauli hizo katika hafla ya mahafali ya 26 ya Chuo cha Kiislamu cha Maahad Imam Shafii, kilichopo Sahare mkoani Tanga, chuo kinachomilikiwa na AMYC.

Akizungumza kama Mgeni Rasmi katika mahafali hayo, Aref Nahdi alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha sekta ya media na kuipa kipaumbele kama nyenzo ya msingi ya kufikisha mafundisho sahihi ya Uislamu kupitia Qur'an Tukufu na Sunnah za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Nahdi, ambaye ana uzoefu mpana katika uendeshaji wa vyombo vya habari, alisema endapo vyombo vya habari vinaweza kutumika vibaya kupotosha jamii, basi vinaweza pia kutumika kwa nguvu ileile kuzuia uovu na kusambaza haki iwapo vitamilikiwa na kusimamiwa kwa misingi sahihi.

The Islamic Foundation ni miongoni mwa taasisi zilizowekeza katika sekta hiyo, kwa kumiliki vyombo mbalimbali vya habari chini ya mtandao wa Imaan, ikiwemo Radio Imaan, TV Imaan, Gazeti Imaan pamoja na majukwaa mbalimbali ya mitandao ya kijamii, ambavyo kwa pamoja vimekuwa na mchango mkubwa katika kueneza da'awah na kuelimisha jamii.

Nahdi ameendelea kusisitiza kuwa chuki na propaganda dhidi ya Uislamu ni miongoni mwa sababu zinazoonesha umuhimu kwa Waislamu kumiliki vyombo vyao vya habari ili kujibu hoja potofu kwa njia ya kielimu, staha na busara.

Kwa upande wake, Sheikh Salim Barahiyan, alisisitiza kuwa kutokana na utandawazi na maendeleo makubwa ya teknolojia, masheikh na walinganiaji wa dini hawana budi kuendana na nyakati kwa kutumia mitandao ya kijamii kama silaha ya kueneza da'awah.

Alisema kupitia mitandao hiyo, walinganiaji wanaweza kuifikia jamii kwa urahisi zaidi na kuinusuru dhidi ya makundi yenye nia ovu yanayotumia majukwaa hayo kueneza upotevu na kuvuruga maadili ya jamii.

"Silaha kubwa ya mapambano kwa zama zetu ni mitandao ya kijamii, kwa sababu tumeshuhudia hata watu wasiokuwa na nia njema na nchi yetu wakitumia mitandao hiyo kushawishi vurugu na maandamano kwa lengo la kuharibu amani," alisema Sheikh Barahiyan.

Sanjari na hayo, alitoa bishara njema ya upatikanaji wa sera ya da'awah ya taasisi ya Ansaar Muslim Youth Centre, itakayogawiwa kwa wahitimu wa chuo hicho ili kuwasaidia wanapoingia katika jamii, ikiwemo kuwaongoza katika matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii kwa ajili ya kueneza da'awah.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Maahad Imam Shafii, Badru Issa Badru, aliwanasihi wahitimu kuwa waangalifu katika matumizi ya mitandao ya kijamii ili wawe chanzo cha athari chanya na manufaa kwa jamii inayowategemea. Katika msisitizo huo huo, Sheikh Ibrahim Twaha, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya The Islamic Foundation, aliwataka wahitimu kutumia mitandao ya kijamii pamoja na tovuti mbalimbali za Kisunnah kwa ajili ya kujifunza zaidi, kupanua uelewa wao wa dini na kusambaza elimu sahihi kwa jamii.

## Nahdi, Sheikh Barahiyan watajwa chachu ya maendeleo ya Uislamu

**Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Sheikh Ibrahim Twaha, amewataka Waislamu nchini Tanzania kuwatambua na kuwapa heshima viongozi wa taasisi mbili kubwa za Kiislamu—Sheikh Salim Barahiyan, Mudir wa Taasisi ya Ansaar Muslim Youth Centre (AMYC), na Aref Nahdi, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation—akisema ni chachu muhimu ya maendeleo ya dini na jamii kwa ujumla.**

**Sheikh Twaha aliyasema hayo katika hafla ya mahafali ya 26 ya Chuo cha Dini cha Maahad Imam Shafii, kilichopo Sahare, mkoani Tanga, ambapo jumla ya wahitimu 70 wa kike na wa kiume walitunukiwa vyeti vya elimu ya dini ngazi ya thanawi.**

**Akiwasilisha salamu zake katika mahafali hayo, Sheikh Twaha—ambaye pia ni mwanadaawah mahiri na Mlezi Msaidizi wa Maahad Imam Shafii—alisema viongozi hao wamefanya kazi kubwa na ya kuigwa katika kusongesha mbele Uislamu kupitia uwekezaji wa elimu, daawah na miradi ya maendeleo ya jamii.**

**Taasisi hizo mbili, ambazo viongozi hao ni waasisi wake, zina rekodi zinazoonesha kuwa ni miongoni mwa taasisi zenye ushawishi mkubwa nchini, zikitekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa misikiti, maahadi, shule na vyuo, uendeshaji wa vyombo vya habari pamoja na miradi ya kijamii kama uchimbaji wa visima vya maji.**

**Sio siri pia kuwa ushirikiano wa karibu kati ya Ansaar Muslim Youth Centre na The Islamic Foundation umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa shughuli za daawah nchini, hasa ukizaingatia kuwa zote ni wanachama waandamizi wa Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA).**

### Historia ya Maahad Imam Shafii

**Historia ya chuo hicho iliguswa na wazungumzaji kadhaa katika mahafali hayo, kila mmoja akiongeza kipande muhimu cha simulizi ya uanzishwaji na maendeleo yake.**

**Sheikh Hassan Mohammed, mmoja wa walimu wa chuo hicho, alisema Maahad Imam Shafii ilianzishwa mwaka 1997, na akaeleza kuwa kipindi cha mwanzo mazingira hayakuwa na vishawishi vingi kama ilivyo sasa, hali iliyowawezesha wanafunzi kujikita zaidi katika kusoma vitabu na kujenga misingi imara ya kielimu na kifikra.**

**Kwa upande wake, Mudir wa chuo, Sheikh Ally Nassor, alisema chuo hicho kimejijengea sifa ya kipekee ya kuzalisha wahitimu wanaoendelea na masomo katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi, na baadhi yao kurejea chuoni hapo kuchangia katika ufundishaji ili kuendeleza elimu ya Sharia.**

شَعْبان

HABARI TANGA

NA BIN HAJJ IBRAHIMU HAJJ

# Wahitimu 70 waagwa Maahad Imam Shafii kwa nasaha nzito

Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, pamoja na Mudir wa Taasisi ya Ansaar Muslim Youth Centre (AMYC), Sheikh Salim Barahiyan, ni miongoni mwa viongozi wakuu walitoa nasaha kwa wahitimu 70 wa Chuo cha Kiislamu cha Maahad Imam Shafii, katika mahafali ya 26 ya chuo hicho yaliyofanyika Sahare, mkoani Tanga.

Viongozi hao wawili, wakifuatana na viongozi waandamizi wa taasisi zao pamoja na wageni waalikwa, walitoa ujumbe unaofanana kwa wahitimu hao wakisisitiza umuhimu wa kujifahamu, kujipamba kwa tabia njema, kuendelea kujifunza, na kuendana na nyakati kwa kutumia nyenzo za kisasa ikiwemo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Mahafali hayo yalianza rasmi kwa usomaji wa Qur'an Tukufu uliosomwa na mwanafunzi wa mwaka wa kwanza ngazi ya mutawasitwa, Yusuf Abdillah, kabla ya kufuatiwa na kalima fupi kutoka kwa Sheikh Hassan Mohammed, mmoja wa walimu wa chuo hicho.

Katika kalima yake, Sheikh Hassan aligusia historia ya uanzishwaji wa Maahad Imam Shafii, akieleza kwa ufupi safari ya chuo hicho tangu kuanzishwa kwake na kukumbusha mazingira ya awali ya masomo, huku akiwahimiza wahitimu kuendeleza juhudi za kielimu na kuyafanyia kazi mafunzo waliyopata.

Baada ya hapo, Mudir wa Chuo cha Maahad Imam Shafii, Sheikh Ally Nassor, alitoa neno la ukaribisho kwa wageni rasmi na waalikwa, akieleza kwa muhtasari upekee wa chuo hicho katika kuandaa wanafunzi wa elimu ya dini na mchango wake kwa jamii tangu kuanzishwa kwake, sambamba na kutoa shukrani kwa taasisi na wadau waliokisaidia.

Sheikh Nassor pia alitumia fursa hiyo kutoa shukrani kwa taasisi na watu binafsi waliokisaidia chuo hicho, akiwemo Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, kwa ushirikiano na misaada iliyochangia maendeleo ya chuo,



kabla ya kumuomba mgeni rasmi kuendelea kukiunga mkono.

Katika mfululizo huo wa nasaha, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya The Islamic Foundation na Mlezi Msaidizi wa chuo, Sheikh Ibrahim Twaha, aliwakumbusha wahitimu umuhimu wa tabia njema na nidhamu, akisisitiza kuwa dini ya Uislamu imekuja kumjenga mwanadamu aishi katika misingi ya maadili ya hali ya juu, si elimu pekee bali pia mwenendo unaoakisi mafundisho ya dini.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Maahad Imam Shafii, Badru Issa Badru, aliwasihi wahitimu kujifahamu, kuwa na mwelekeo wa maisha, na kuwa waangalifu katika matumizi ya mitandao ya kijamii ili wawe chanzo cha athari chanya na manufaa kwa jamii inayowategemea.

Kisha ulifika wakati wa Sheikh Barahiyan, ambaye pia ni mwenyeji wa hafla hiyo, aliytetoa kalima fupi iliyogusia kwa ujumla malengo ya kuanzishwa kwa chuo hicho, ikiwa ni kuwaandaa maimamu na walinganiaji watakaolitumikia Umma kwa elimu, busara na uadilifu, huku akiwahimiza wahitimu kuendana na changamoto za zama walizo nazo.

Hatimaye, Mgeni Rasmi, Aref Nahdi, alihitimisha mahafali hayo kwa nasaha nzito, akiwataka wahitimu kujipamba kwa tabia njema na kuahidi kuwa Taasisi ya The Islamic Foundation itaendelea kuwa mstari wa mbele kutoa ushirikiano kwa wahitimu watakaojitokeza kwa mwenendo na matendo mema.

Aidha, aliwataka wahitimu kuwa mabalozi wa amani na maridhiano, wakisaidia kupunguza malumbano ya masheikh ndani ya jamii kwa kuwashauri kwa hekima pale kauli zisizo sahihi zinapotolewa na kusababisha taharuki na mgawanyiko.

Akigusia upande wa wahitimu wa kike, Nahdi alisema wanawake wasomi wa dini wana nafasi na mchango mkubwa katika jamii, akibainisha kuwa wao ni walezi katika familia na wana ushawishi mkubwa katika malezi ya vizazi vijavyo.

"Nawahusia sana ndugu zangu wakinamama mjipambe kwa tabia njema, na msiwe sababu ya kuivuruga jamii kwa kufanya matendo yasiyofaa ikiwemo kuvaa mavazi yasiyo ya stara kisheria, kwani hakika nyinyi mna ushawishi mkubwa katika kuijenga jamii au kuibomoa," alisema Nahdi.

Hafla hiyo ilifikia tamati kwa neno la shukrani lililotolewa na Katibu Mkuu wa Taasisi ya Ansaar Muslim Youth Centre, aliyewashukuru viongozi, wageni na washiriki wote kwa kushiriki mahafali hayo ya kihistoria.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

## Wahitimu 70 waagwa Maahad Imam Shafii kwa nasaha nzito











KUELEKEA Ramadhan

NA YUSUPH AMIN



# Serikali yaonya wanaopandisha bei za bidhaa

Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba amewataka wafanyabiashara nchini kuacha kuwaumiza Watanzania kwa kupandisha bei za bidhaa katika kipindi hiki cha kuelekea Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, akisisitiza kuwa nchi haina uhaba wa chakula na kuna ziada ya kutosha.

Akizungumza Bungeni wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kuhusu uhaba wa mvua, Dkt. Mwigulu alisema kuwa licha ya tahadhari ya upungufu wa mvua iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Tanzania ina akiba ya chakula zaidi ya tani 400,000 ikilinganishwa na hitaji la kitaifa la tani 150,000.

"Kwa sasa tunayo akiba ya chakula cha kutosha, hakuna sababu ya bei kupanda," alisema Waziri Mkuu na kuwataka Wakuu wote wa Mikoa nchini kuendelea kuwaelimisha wananchi kutunza na kutumia chakula kwa busara ili kuongeza akiba.

Waziri Mkuu alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Nancy Nyalusu, aliyetaka kufahamu mipango ya Serikali katika kuhakikisha uhaba wa chakula haujitokezi wakati wa mfungo wa mwezi wa Ramadhan.

## ...Dkt. Mwinyi: Hakuna sababu ya kupandisha bei ya bidhaa



Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi amesema Zanzibar haina uhaba wa bidhaa za chakula, hivyo wafanyabiashara hawana sababu ya kupandisha bei wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Rais Mwinyi aliyasema hayo Ijumaa iliyopita wakati alipojumuika na Waumini wa Dini ya Kiislamu katika ibada ya sala ya Ijumaa iliyofanyika kwenye msikiti wa Fatma Bint Issa, Kidongo Chekundu, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Katika hotuba yake, Rais Dkt. Mwinyi alisema Serikali imetoa maelekezo kwa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kuhakikisha bei za mchele, unga wa ngano na sukari hazipandishwi kwa kuwa zinapatikana kwa wingi.

Alisisitiza kuwa Ramadhan ni mwezi wa rehema na kusaidiana, si mwezi wa kuongeza bei za bidhaa za vyakula, hivyo amewahimiza Waumini kusaidiana na kuwasaidia wasio na uwezo sambamba na kujiandaa vema kuupokea Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

شَعْبان

# HABARI
## DAR ES SALAAM

MWANDISHI WETU



# Rais Samia azuru UAE kushiriki World Government Summit

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiondoka nchini kuelekea Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) tarehe 02 Februari, 2026, ambapo atashiriki kwenye mkutano wa World Government Summit (WGS 2026) na uzinduzi wa Global Africa Investment Summit (GAIS).**

**Ushiriki wa Tanzania katika WGS 2026 unaakisi utekelezaji wa DIRA 2050 na Sera Mpya ya Mambo ya Nje, zinazoweka diplomasia ya kiuchumi kama nguzo ya mahusiano ya kimataifa. Lengo ni kuoanisha sera, ushirikiano na mitaji ya uwekezaji kwa maendeleo ya taifa.**

MAHMOUD NYAMGUMA

# Saudi Arabia yasisitiza wao na UAE ndugu, kuendelea kutetea Wapalestina



**Mwenyekiti wa Kituo cha Utafiti wa Mfalme Faisal na aliyewahi kuwa balozi, Mwanamfalme Turki Al-Faisal, amesema tofauti za maoni ni za kawaida ndani ya GCC lakini haziwezi kuvunja misingi ya udugu wa kidini, kifamilia na kihistoria kati ya mataifa hayo mawili.**

Saudi Arabia imethibitisha tena msimamo wake wa mshikamano wa Kiislamu na uthabiti wa kikanda, ikisisitiza uhusiano wa kindugu na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) huku ikitetea haki za Wapalestina kama msingi wa amani ya kweli.

Akizungumza katika mkutano wa "Investing is a Sea," na kunukuliwa na Arab News, Mwenyekiti wa Kituo cha Utafiti wa Mfalme Faisal na aliyewahi kuwa balozi, Mwanamfalme Turki Al-Faisal, amesema tofauti za maoni ni za kawaida ndani ya GCC lakini haziwezi kuvunja misingi ya udugu wa kidini, kifamilia na kihistoria kati ya mataifa hayo mawili.

Turki alitoa wito kwa wananchi kurejea vyanzo rasmi vya habari badala ya propaganda za mitandao ya kijamii, akibainisha kuwa kelele za mtandaoni kuhusu Yemen zimechochewa na taarifa potofu.

Takwimu za vyombo huru zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya mijadala ya mtandaoni kuhusu mvutano wa kikanda mwaka 2025 zilitokana na akaunti zisizo rasmi, hali inayodhoofisha mshikamano wa Kiislamu.

Saudi Arabia, kupitia viongozi wake, imesisitiza kuwa uhusiano wake na UAE umejengwa juu ya "mafungamano, si mgongano," kwa maslahi ya Ummah na usalama wa Ghuba.

Wakati huo huo, Mwanamfalme Turki amesisitiza kuwa haki ya kujilinda haiwezi kutolewa upande mmoja wa Israel pekee huku Wapalestina wakinyimwa haki hiyo.

Akirejea ziara ya Mrithi wa Kiti cha Enzi Mohammed bin Salman, mjini Washington, Prince Turki amesema msimamo wa Ufalme ni wazi: hakuna uhalalishaji wa Israel bila kuanzishwa kwa dola huru ya Palestina.

Kauli hii inaungwa mkono na nchi nyingi, ambapo kura za Baraza Kuu la UN zimeonesha zaidi ya nchi 140 ziko upande wa Wapalestina. Saudi Arabia inaona hili kama jukumu la kidini na kimaadili kwa Ummah.

Taarifa za mashirika ya kimataifa zinaonesha kuwa tangu Oktoba 2023, zaidi ya Wapalestina 71,000 wameuawa Gaza na Ukingo wa Magharibi, wengi wao raia, hali inayothibitisha wito wa Saudi Arabia kwamba amani lazima ijengwe juu ya haki na si misingi teule. Katika wakati ambapo mkataba wa amani wa Trump ukiendelea kutekelezwa mashambulizi ya Israel Gaza na Uvamizi wa Wazayuni umeendela kushuhudiwa na kusababisha vifo kwa Wapalestina zaidi ya 450 na mamia kuhamishwa makazi yao katika ukingo wa magaharibi.

MWANDISHI WETU

# Samia: Fanyeni upandaji wa miti kuwa sehemu ya mipango ya miji

Rais Samia Suluhu Hassan amezitaka mamlaka za upimaji ardhi na mipango miji kuhakikisha kuwa maendeleo mapya yanatenga maeneo ya kupanda miti kama sehemu ya mipango ya makazi na matumizi ya ardhi.

Pia amezihimiza taasisi za umma na binafsi kupanda angalau mti mmoja katika maeneo yao na kuhakikisha unatunzwa ipasavyo hadi ukubwani, kama hatua ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Rais aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya siku yake ya kuzaliwa ya miaka 66, yaliyohusisha upandaji wa mti wa kumbukumbu na kukata keki.

"Nazihimiza mamlaka za ardhi na mipango miji kote nchini kuhakikisha kuwa viwanja vipya vinajumuisha maeneo ya kijani na nafasi za kupanda miti katika mipango ya makazi na matumizi ya ardhi," alisema.

Rais Hassan alisisitiza kuwa mabadiliko ya tabianchi si suala la kinadharia tena bali ni uhalisia unaoathiri maisha ya kila siku. Alitaja changamoto kama mvua zisizotabirika, ukame, mafuriko, kuongezeka kwa joto na kupanda kwa kina cha bahari kama matatizo yanayoikumba dunia, akibainisha kuwa Tanzania nayo haiko salama. Nchini, mabadiliko ya tabianchi yanaathiri moja kwa moja maisha ya wananchi, ikiwemo upatikanaji wa maji salama na uzalishaji wa chakula.

Alieleza kuwa upandaji miti ni suluhisho muhimu, akisisitiza kuwa miti inayopandwa leo itanufaisha vizazi vijavyo. Aliwataka viongozi wa mikoa na wilaya katika maeneo yaliyoathirika kusimamia kikamilifu shughuli za upandaji miti badala ya kusubiri matukio ya ishara tu.

"Kupanda miti ni sehemu ya wajibu wetu wa kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ajili ya vizazi vijavyo. Tumerithi misitu yenye utajiri, ardhi yenye rutuba na miti ya matunda inayozalisha; ni jukumu letu kuitunza na kuikuza," alisema.

Rais Hassan aliunganisha upandaji miti na Malengo kadhaa ya Maendeleo Endelevu (SDGs), ikiwemo SDG 13 kuhusu hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, SDG 15 kuhusu uhai wa nchi kavu, SDG 2 ya kutokomeza njaa, SDG 3 kuhusu afya na ustawi, SDG 6 kuhusu maji safi, na SDG 1 ya kupunguza umaskini.

Alisema Tanzania imejidhatiti kushiriki katika jitihada za kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo Mkataba wa Paris unaotaka hatua za pamoja za kupunguza uzalishaji wa hewa chafu. Pia alitaja wilaya zinazofaidika kiuchumi na shughuli za misitu, kama uzalishaji wa mbao na miradi mingine inayotokana na misitu.

Akieleza athari za upandaji miti kwa wingi, Rais alisema iwapo Watanzania milioni 30 kila mmoja angepanda mti mmoja kila mwaka, nchi ingeweza kufanikisha urejeshaji mkubwa wa misitu ndani ya miaka michache. Aliwataka wananchi wote kushiriki kikamilifu, akisisitiza ulinzi wa mazingira na uzalendo.






MWANDISHI WETU

# Mwinyi ahimiza umuhimu kujipamba na Qurani, malezi bora kwa vijana

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewataka Waumini wa Dini ya Kiislamu kujipamba na Qurani Tukufu, kuishi kwa kufuata miongozo na mafundisho yake pamoja na kuifanya Qurani kuwa dira ya maisha yao ya kila siku.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema aliposhiriki Mashindano ya Kimataifa ya Kuhifadhi Qurani, yaliyoandaliwa kwa ushirikiano wa Taasisi ya Altijarah Al Arabia ya Oman na Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, yaliyofanyika katika Msikiti wa Jamiu Zanzibar, Kiembe Samaki, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi amewanasihi Waumini wa Dini ya Kiislamu pamoja na Wananchi kwa ujumla kushikamana, kuishi kwa umoja, kusaidiana na kudumisha maadili mema ili kupata baraka za Mwenyezi Mungu.

Halikadhalika, amesisitiza umuhimu wa kuishi kwa kupendana, kuimarisha malezi bora ya vijana pamoja na kulinda amani na utulivu wa nchi, akieleza kuwa misingi hiyo ni nguzo muhimu ya maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Rais Dkt. Mwinyi ameipongeza Taasisi ya Altijarah Al Arabia ya Oman pamoja na Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kwa kufanikisha mashindano hayo, pamoja na mchango wao mkubwa katika kuihudumia jamii kupitia sekta za elimu, afya, chakula na huduma za kijamii kupitia kambi mbalimbali. Amesisitiza umuhimu wa kuendeleza na kuimarisha ushirikiano kati ya Taasisi hizo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Vilevile, Rais Dkt. Mwinyi amewapongeza washiriki wa mashindano hayo na kuwahimiza kuendelea kushikamana na Qurani Tukufu sambamba na taaluma walizonazo ili kufanikisha mafanikio zaidi duniani na Akhera.

Mashindano hayo ya Kimataifa yamehusisha washiriki sita kutoka nchi za Ujerumani, Uganda, Tanzania, Urusi, Canada na Brazil, ambapo mshiriki Ndg. Usama Barghouth kutoka Ujerumani ameibuka mshindi wa kwanza na kutunukiwa kombe, cheti pamoja na zawadi ya shilingi milioni 20.






HABARI DODOMA

UKHTI FATIMA SS

# Bajeti ya kihistoria ya Sh 62 trilioni kwa mwaka wa fedha 2026/27 yazinduliwa

## Ni Bajeti ya kupunguza Utegemezi wa fedha za nje

Serikali inatarajia kutegemea zaidi mapato ya ndani kufadhili bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2026/27, hali inayoonesha mwelekeo wa kupunguza utegemezi wa misaada ya nje na kuimarisha uhimilivu wa fedha kitaifa.

Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27 inatarajiwa kuwa Sh61.93 trilioni. Kati ya fedha hizo, mapato yote yanayotarajiwa kukusanywa, ikijumuisha misaada ni Sh46.69 trilioni, sawa na asilimia 75.4 ya bajeti yote.

Mapato ya kodi yanakadiriwa kuwa Sh36.89 trilioni huku mapato mengine yakifikia Sh9.24 trilioni yakiwemo mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Sh1.97 trilioni. Kwa ujumla, mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia Sh46.13 trilioni, sawa na takribani asilimia 74.5 ya bajeti kuu ya Serikali kwa mwaka huo wa fedha.

Ongezeko hili la ufadhili wa bajeti ya ndani linatarajiwa kuwa la juu zaidi katika kipindi cha miaka minne iliyopita kwani kwa mujibu wa bajeti ya Serikali mwaka 2022/23 makadirio ya makusanyo ya ndani yalikuwa asilimia 67.6, mwaka uliofuata ikiwa asilimia 70.7 na 2024/25 ilikuwa asilimia 72.6.

Vilevile, mwaka wa fedha unaoendelea wa 2025/26 Serikali ilikadiria mapato na matumizi kuwa Sh56.49 trilioni na makusanyo kuwa Sh40.47 trilioni sawa na asilimia 71.6 ya bajeti kuu.

Kwa upande mwingine, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inakadiriwa kuwa Sh563.1 bilioni pekee, sawa na asilimia 0.9 ya bajeti yote, hali inayoonesha utegemezi mdogo wa misaada ikilinganishwa na mapato ya ndani.

Kwa mtazamo wa kina zaidi, mapato ya kodi pekee yanatarajiwa kugharamia asilimia 59.6 ya bajeti ya Serikali, jambo linaloonesha uzito mkubwa wa kodi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali na utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Fedha, Balozi Hamis Mussa Omary alipowasilisha bungeni mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati 2026/27 hadi 2028/29. Alisema ongezeko la mapato ya ndani linatarajiwa kuchangiwa na misingi imara ya uchumi jumla na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ikiwemo kuhimiza matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) katika malipo na ukusanyaji wa mapato.

Pia, alisema Tehama inatumika katika kudhibiti misamaha ya kodi, kurasimisha sekta isiyo rasmi, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuibua vyanzo vipya vya mapato.

Katika kipindi cha muda wa kati kuanzia 2026/27 hadi 2028/29, alisema Serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh204.09 trilioni, sawa na wastani wa Sh68.03 trilioni kwa mwaka, huku mapato yakikadiriwa kufikia wastani wa Sh52.48 trilioni kwa mwaka, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 12.1.

"Hatua hizi zinaendana na malengo ya uchumi jumla yanayolenga mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na wastani wa asilimia 17.2 katika kipindi cha muda wa kati, pamoja na kudhibiti nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa," alisema.

Kwa ujumla, takwimu hizi zinaonesha kuwa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27 imejengwa kwa msingi mkubwa wa mapato ya ndani, ishara ya mkakati wa Serikali wa kuimarisha uhuru wa kifedha na uendelevu wa matumizi ya umma.



Waziri wa Fedha, Balozi Hamis Mussa Omary akiwasilisha bungeni mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati 2026/27 hadi 2028/29.

UKHTI FATIMA SS




# Hisa za makampuni mawili tu zakidhi vigezo halal DSE




Hisa mbili pekee, Twiga Cement (TPCC) na Swissport Tanzania (SWIS) ndizo zimebainika kukidhi vigezo vya uwekezaji wa kihalal katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), baada ya uchujaji wa Sharia kuonyesha kuwa chaguo la hisa "halal" bado ni finyu nchini.

Hayo yameelezwa kwenye Ripoti ya mwaka 2025 ya Shirkah 2025, inayosema kuwa DSE ina hisa 28, lakini ni hisa tisa tu zilizopita uchujaji wa shughuli za biashara, hisa tatu zikapita uchujaji wa kifedha, na hatimaye mbili pekee zikabaki kuwa "investable" (TPCC na SWIS).

Kwa upande wa kikanda, ripoti inaonesha kuwa Kenya kupitia Nairobi Securities Exchange (NSE) ina baadhi ya hisa zinazoonesha hadhi ya "halal" ikiwemo Safaricom (SCOM) na AMAC, wakati Uganda Securities Exchange (USE) ikionyesha hisa kama MTN Uganda (MTNU) na QCIL zikiwa kwenye kundi la "halal" katika jedwali la uchambuzi wa soko.

Kuhusu mapendekezo ya uwekezaji, Shirkah imeshauri hisa zilizokidhi vigezo—SWIS na TPCC—ziwe kwenye mkakati wa "Buy/Hold", ilhali hisa zisizokidhi vigezo kama TOL Gases na Vodacom Tanzania zimepewa ushauri wa "Sell and purify" (uza na fanya utakaso wa mapato).

Ripoti inaeleza kuwa uhalalali wa hisa huamuliwa na vigezo viwili vikuu: (i) uchujaji wa sekta/aina ya biashara ili kampuni isijihusishe na shughuli zisizokubalika kimaadili na kisharia, na (ii) uchujaji wa viashiria vya kifedha ili kampuni isizidi viwango vinavyokiuka misingi ya uwekezaji wa halal.

Katika eneo la sukuk, ripoti inaonyesha kuwa Tanzania imejenga msingi wa soko la sukuk kupitia uwepo wa sukuk zaidi ya 10 za kampuni binafsi, sukuk 1 ya kampuni iliyoorodheshwa, pamoja na sukuk 1 ya quasi-sovereign, na sukuk 1 iliyokwisha kulipwa (redeemed), ikionyesha ukuaji wa bidhaa mbadala za fedha zisizo za riba.

Kwa sasa, "Islamic finance landscape" nchini Tanzania inaainishwa na kuwepo kwa benki 5 za Kiislamu zenye takribani asilimia 5 ya mali za sekta ya benki, waendeshaji 2 wa takaful, na mifuko 2 ya halal, sambamba na kuwepo kwa miongozo ya sukuk na kanuni za benki zisizo na riba.

Kwa mtazamo wa kimataifa, ripoti pia inaonyesha ukuaji wa sekta ya fedha za Kiislamu duniani, ikitaja, miongoni mwa takwimu zake, ongezeko la utoaji wa sukuk na kuongezeka kwa mvuto wa bidhaa za halal katika masoko mbalimbali, jambo linaloashiria mazingira mapana yanayoweza kuifanya Afrika Mashariki kuvutia mitaji ya kimaadili.

Shirkah ni kampuni inayojihusisha na uwekezaji wa halal katika madaraja mbalimbali ya mali ikiwemo hisa, sukuk, soko la fedha, mifuko ya halal, majengo, bidhaa na hata biashara changa za ubunifu, ikilenga zaidi masoko ya EAC na SADC.

## Changamoto

Ni wazi kuwa pamoja na hatua zilizopigwa, sekta ya uwekezaji wa kihalal nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla bado inakabiliwa na changamoto kadhaa. Changamoto kuu ni idadi ndogo ya hisa zinazokidhi kikamilifu vigezo vya Sharia, hususan katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, ambako ni hisa mbili pekee kati ya 28 ndizo zilizoonekana kufaa kwa uwekezaji wa halal.

Kampuni nyingi bado zina miundo ya kifedha inayotegemea deni la riba, jambo linalozifanya kushindwa kupita uchujaji wa kifedha wa Sharia. Aidha, kuna uhaba wa bidhaa mbadala kama mifuko mingi ya halal na hisa mpya zinazozingatia maadili, hali inayopunguza chaguo kwa wawekezaji.

Ripoti pia inataja uelewa mdogo wa umma kuhusu uwekezaji wa kihalal na gharama za kuzingatia matakwa ya udhibiti kama vikwazo vinavyohitaji kushughulikiwa kupitia elimu ya kifedha, ubunifu wa bidhaa na ushirikiano wa karibu kati ya wadhibiti, masoko ya mitaji na taasisi za fedha za Kiislamu.

MWANDISHI WETU

# Zanzibar kuimarisha utoaji haki kiteknolojia

**Uzinduzi wa mfumo huo unatarajiwa kufanyika Februari 9, 2026 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi kisiwani Pemba, ikiwa ni kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria Zanzibar, ambapo utafanywa na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi.**

Mahakama Kuu ya Zanzibar inatarajia kuzindua mfumo wa kisasa wa usikilizaji wa kesi na usimamizi wa mashauri kwa njia ya kielektroniki, hatua inayolenga kuimarisha utoaji wa haki kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama).

Uzinduzi wa mfumo huo unatarajiwa kufanyika Februari 9, 2026 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi kisiwani Pemba, ikiwa ni kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria Zanzibar, ambapo utafanywa na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdulla, kuanzishwa kwa mfumo huo wa kielektroniki kutasaidia kesi zote kusikilizwa kwa kutumia teknolojia, jambo litakalopunguza changamoto za ucheleweshaji wa mashauri na kuongeza uwazi katika utoaji wa haki.

"Mfumo huo utawezesha usimamizi bora wa mashauri kuanzia usajili wa kesi, upangaji wa tarehe za kusikilizwa, hadi ufuatiliaji wa maamuzi kwa njia ya kidijitali," alisema.

Alifafanua matumizi ya teknolojia katika mahakama yataongeza ufanisi wa kazi, kupunguza gharama kwa wananchi na taasisi za haki, pamoja na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimahakama.

Kwa mujibu wa Jaji mkuu huyo, hatua hiyo ni sehemu ya mageuzi makubwa yanayofanywa na Mahakama ya Zanzibar ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na mahitaji ya jamii ya sasa.

Maadhimisho ya wiki ya Sheria Zanzibar yanalenga kuhimiza matumizi ya Tehama katika utoaji wa haki, kuimarisha huduma kwa wananchi na kujenga mfumo wa mahakama wenye ufanisi na uwajibikaji.

Aliongeza kuwa maadhimisho hayo ni jukwaa muhimu la kuwakutanisha wadau wa haki ili kujadili masuala mbalimbali yanayohusu utawala wa sheria na kubadilishana uzoefu wa kitaaluma.

Jaji Ramadhan alisema kupitia maadhimisho hayo, Mahakama hupata fursa ya kutathmini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo pamoja na kuweka mikakati ya kuboresha huduma za haki kwa wananchi.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria kwa mwaka huu yanafanyika chini ya kaulimbiu isemayo "Matumizi ya Tehama ni chachu ya upatikanaji wa haki."

Kwa mujibu wa Jaji Ramadhan, kaulimbiu hiyo inaakisi dhamira ya Serikali katika kuimarisha mifumo ya haki kwa kutumia teknolojia.

Hata hivyo, alisema katika kipindi cha maadhimisho hayo, kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwemo makongamano ya kitaaluma yanayowakutanisha wataalamu wa sheria na wadau wa sekta ya haki.

Shughuli nyingine zitakazofanyika ni utoaji wa elimu ya haki kwa jamii, lengo likiwa ni kuwawezesha wananchi kufahamu haki zao za msingi na taratibu za kisheria, pia kutakuwa na maonyesho ya huduma za kimahakama pamoja na ushiriki wa taasisi mbalimbali za haki zitakazowasilisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi.



KUELEKEA Ramadhan

NA ZAHARANI BARAKA

# Maisha ya Mtume katika mwezi wa Shaaban

Aghlabu watu wengi huupuuza mwezi wa Shaaban licha ya kuwa na fadhila nyingi na fursa adhimu za kutubu na kujikurubisha kwa Allah Mtukufu. Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa kielelezo chema kwetu katika kutumia nyakati zote kwa ibada, na wakati huohuo akiupa umuhimu mwezi wa Shaaban na kuutofautisha na miezi mingine kwa kujikurubisha zaidi kwa Allah Mtukufu.

Imepokewa hadith kutoka kwa mama Aisha (Allah amridhie) akisema: "Sijamuona Mtume akifunga mwezi mzima kama alivyokuwa akifunga Ramadhan, na sijamuona akifunga (Sunna) mara nyingi kama alivyofunga katika (mwezi wa) Shaaban." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii tukufu inaonesha namna Mtume (rehema na amani zimshukie) alivyoupa umuhimu maalum mwezi wa Shaaban, kwani alikuwa akizidisha kufunga Sunna kuliko miezi mingine.

Funga hii haikuwa ni utekelezaji wa sharia tu, bali ilikuwa ni kielelezo cha imani ya kina na hamu ya dhati ya kujikurubisha kwa Allah Mtukufu pamoja na kujiandaa na mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Kufunga katika mwezi wa Shaaban ni mazoezi ya kiroho na kimwili ya kujiandaa na swaumu ya Ramadhan pamoja na kuuandaa moyo na roho kuupokea mwezi huo kwa ari ya juu kabisa.

Mazoezi haya ya kiroho hayakuwa katika swaumu peke yake bali yalihusisha pia ibada za sala nyakati za usiku (Qiyamu Llayl), kufanya Adhkaar mbalimbali na kuomba dua. Hizi zote ni ibada zinazomkurubisha mja kwa Mola wake na kumuongezea unyenyekevu na uchamungu.

Hivyo basi, mwezi wa Shaaban ni fursa nzuri ya kuongeza bidii katika ibada hizi ili kufikia daraja za juu za uchamungu na ikhlas. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema mwezi wa Shaaban ni daraja la kupita kuielekea Ramadhan. Kama ambavyo msafiri anajiandaa kwa safari ndefu ndivyo Muislamu anavyopaswa kujiandaa kimwili na kiroho kwa ajili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akijiandaa na Ramadhan ndani ya mwezi wa Shaaban kwa kuongeza juhudi katika ibada. Kwa waumini, hii ni fursa ya dhahabu ya kuzitakasa nafsi dhidi ya madhambi na makosa, kumuomba Allah msamaha na kutubia kwake, na kuanza ukurasa mpya ulio safi.

Na toba ya kweli ni kurejea kwa Allah baada ya kufanya kosa (dhambi) kwa nia ya dhati ya kutorudia tena kosa. Toba hufuta madhambi na makosa na humrudisha mja katika radhi za Mwenyezi Mungu. Anayeomba msamaha katika mwezi wa Shaaban hujiandaa na Ramadhan na kuupokea mwezi huo Mtukufu kwa moyo msafi na nafsi yenye utulivu.

Kwa hakika maandalizi huufanya mwezi wa Ramadhan kuwa wa baraka, kwani Muislamu huhisi ladha ya ibada na kuvuna matunda yake kikamilifu. Ama yule anayeingia Ramadhan bila maandalizi anaweza kukosa fadhila nyingi na asifikie malengo yanayokusudiwa ya mwezi huu Mtukufu, yaani uchamungu.

Hata hivyo, ieleweke wazi kwamba kuongeza ibada katika mwezi wa Shaaban haimaanishi kujipa uzito kupita kiasi au kufanya juhudi zilizopitiliza katika ibada kiasi cha kusababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia.

Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa mfano bora katika kufanya mambo



kwa wastani (kati na kati), na alikuwa akionya dhidi ya kupitiliza na kujikaza kupita kiasi. Kinachotakiwa ni kuongeza matendo mema kadiri inavyowezekana bila kuichosha nafsi au kupuuza majukumu mengine ya maisha.

## Kuzingatia fadhila za mwezi huu

Licha ya fadhila zake kutotajwa sana kama ilivyo kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, mwezi wa Shaaban una fadhila nyingi na kubwa. Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akizidisha dua katika mwezi huu. Hii inaonesha umuhimu wa mwezi wa Shaaban, kwamba si mwezi wa kawaida bali ni mwezi wenye fursa kubwa ya kutubu, kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kuomba dua.

Kuomba dua katika mwezi huu ni miongoni mwa matendo bora, kwani Mwenyezi Mungu ni Mkarimu na Mwenye Rehema, anaitikia dua za waja wake waumini hasa katika nyakati zenye baraka.

## Matendo kunyanyuliwa

Shaaban ni mwezi ambao ndani yake matendo ya waja huinuliwa kwenda kwa Allah Mtukufu. Imepokewa hadith kutoka kwa Usama bin Zayd (Allah amridhie) akieleza kuwa, Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "(Shabaan) ni mwezi ambao ndani yake matendo yanapandishwa kwa Mola wa walimwengu wote. Nami napenda matendo yangu yapandishwe hali ya kuwa nimefunga." [Tirmidhi na Nasaiy].

Katika mwezi wa Shaaban, Allah Mtukufu huwatunuku waja wake zawadi kubwa ya kuinuliwa matendo yao kwake, kisha hukubali yale anayoyataka miongoni mwa matendo hayo. Hapa panahitajika kusimama na kujitathmini kielimu na kimaadili.

Ndugu yangu Muislamu, mwezi wa Shaaban ni msimu wa kufungwa daftari lako la matendo na mavuno ya kazi zako za mwaka mzima. Sasa jiulize, mwaka wako utafungwa kwa matendo gani? Hakika maisha aliyoishi Mtume (rehema na amani zimshukie) katika mwezi wa Shaaban ni mfano unaopaswa kuigwa katika kutumia fursa kubwa za kujikurubisha kwa Allah Mtukufu.

Mtume hakuupuuza mwezi wa Shaaban, bali aliongeza ibada ndani yake na kujiandaa kwa ajili ya Ramadhan kwa kiwango cha juu kabisa. Hivyo, nasi tunatakiwa kumuiga Mtume katika mwezi huu wa Shaaban kwa kuongeza juhudi katika ibada, kutubia na kumuomba Allah msamaha.

MWANDISHI WETU

# Dk Mwigulu awakingia kifua wazee

Waziri Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba ameonya tabia ya vijana kujibizana na kuwakejeli wazee, akisema vitendo hivyo vinavunja heshima na ni hatari kwa maadili katika jamii.

Mtendaji mkuu huyo wa Serikali ambaye, kwa nafasi yake, ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM), amesisitiza ni jambo la hatari kwa Taifa unapofika wakati vijana wanapata ujasiri wa kuwavunjia heshima wazee au viongozi wa kiroho.

Kauli ya Dk Mwigulu inakuja wakati ambao kumeshuhudiwa matukio mbalimbali ya vijana, hususan wa kisiasa na wanaharakati, kujibizana na wazee, wakati mwingine hata kutoleana lugha chafu.

## Onyo la Dk Mwigulu

"Ni jambo la hatari kwenye Taifa watu wakiwa na ujasiri wa kufanya kitu ambacho kinavunja heshima dhidi ya Askofu, watu wakakejeli mpaka viongozi wa dini, Sheikh au Mufti. Ni jambo la hatari. Mzee anatokea, mzee mtu mzima, mstaafu au ambaye kwa rika hulingani naye alisema jambo, unajibu kama ni mwanarika mwenzako," alisema.

Aliwataka vijana hao wasitumie kigezo cha siasa kuwajibu wazee hao akisema: "Anatokea tu mzee amefanikiwa katika shughuli zake, tena halazimiki kusema alifanyaje. Naweza nikatoa hata mfano kwa sababu siyo jambo baya kutolea mfano mzee tunayemheshimu."

Alimtolea mfano Mwenyekiti wa Kampuni ya Azam, Said Salim Bakhresa, akisema anaeleza alikopita kwa kuuza bidhaa mbalimbali ndogo hadi kufikia kuwa mwekezaji, lakini anatokea kijana anaandika kukejeli.

Dk Mwigulu alisema wengine wanaandika vitu hata wasivyovijua, baadhi wanawajibu hata wataalamu wa mambo kama sheria, ilhali wao hawana taaluma hizo.

"Jambo la kiuchumi yeye yuko tu pale anamjibu Gavana wa Benki Kuu, Profesa wa uchumi. Huu uharaka wa kuandika kila kitu unakuta neno limetolewa na kiongozi wa kiroho anajibu kama anamuongelea mwizi wa mtaani. Haya si mambo mazuri kwa uelekeo wa Taifa letu," alisema.

Alisema ni hatari vijana wanapojibizana na viongozi wa kiroho kwa sababu wanaheshimiwa na wengine, hivyo ni muhimu kuwa na tahadhari.

"Kama una maoni mazuri sana, kaongelee kuhusu imani yako chumbani kwenye kikao chenu. Ongeeni hapo kama mnavyopanga kuhusu jengo, mnaweza kukaa kama kamati ya ujenzi mkazungumza, lakini usiguse imani ya mwenzako anayoiamini," alisema.



Alisema watu wakizidi kuingiliana kwenye imani, hapatakuwa na mshindi kwa sababu kila mtu jambo moja analoapa kulifia ni lile la kumpeleka mbinguni.

Aidha, kiongozi huyo aliziomba taasisi za dini, viongozi wa rika na jamii kuwekeza katika malezi ya vijana na watoto, akisema matokeo hasi yameanza kuonekana kwenye malezi ya vijana hao.

Alisema zamani malezi yaliyokuwa yakitolewa kwa vijana na watoto yamesaidia hadi sasa Taifa lina watu wanaoheshimiana, hawabaguani kwa kabila, dini au vipato.

Katika hatua nyingine, akiwasilisha salamu za Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu ujenzi wa kanisa hilo, Dk Mwigulu alisema amechangia Sh50 milioni huku yeye mwenyewe akichangia Sh20 milioni kwa ajili ya ujenzi huo.

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




# Asia-Pacific yaongoza soko la chakula cha halal duniani

Ukanda wa Asia-Pacific unaendelea kuongoza kwa ukubwa wa soko la chakula na vinywaji vya halal duniani, huku Ulaya na Afrika vikifuatia kwa kasi.

Ripoti mpya ya Research and Markets iliyochapishwa katika tovuti ya GlobeNewswire inaeleza kuwa soko la chakula na vinywaji vya halal duniani linatarajiwa kukua kutoka dola bilioni 876.74 mwaka 2026 hadi dola trilioni 1.30 ifikapo 2031, sawa na kiwango cha ukuaji wa wastani cha asilimia 8.24 kwa mwaka.

Ukuaji huo unachangiwa na ongezeko la idadi ya Waislamu duniani, linalokadiriwa kufikia karibu watu bilioni mbili, pamoja na kuongezeka kwa mvuto wa bidhaa za halal miongoni mwa wasio Waislamu wanaoziona kama salama, zenye maadili na ubora wa juu.

Kwa mujibu wa Research and Markets, bidhaa za chakula cha halal zilizofungashwa kama vyakula vilivyo tayari kuliwa, bidhaa za mikate na nyama iliyogandishwa ndizo zinazoongoza, huku vinywaji vya halal, ikiwemo maziwa mbadala na vinywaji vya afya, vikikua kwa kasi zaidi.

Soko la vinywaji vya halal linakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 8.78.




Asia-Pacific inaongoza kutokana na miundombinu imara ya uthibitishaji wa halal, huku Ulaya na Afrika zikinufaika na sera za serikali na ongezeko la mahitaji ya watumiaji.

## Nigeria yatajwa kupitwa fursa za uchumi wa halal

**LAGOS,– Licha ya kuwa na zaidi ya Waislamu milioni 100, Nigeria inaendelea kuwa mtumiaji wa pembeni katika uchumi wa Halal wa dunia unaokadiriwa kuzidi dola trilioni mbili, huku masomo ya uchumi huo yakikosekana karibu kabisa katika mitaala ya shule za biashara, kwa mujibu wa mchambuzi Gift Ifeanyi.**

**Ifeanyi anaeleza kuwa Halal si suala la chakula pekee, bali ni mfumo mpana wa viwango unaojumuisha usindikaji wa chakula, fedha za Kiislamu, mitindo ya mavazi ya staha, vipodozi na utalii rafiki kwa Waislamu.**

**Anasema sekta ya chakula pekee ilifikia thamani ya dola trilioni 1.97 mwaka 2025, huku fedha za Kiislamu zikitoa mbadala wa kimaadili katika mazingira ya riba kubwa.**

**Kwa mujibu wa Ifeanyi, nchi zisizo na Waislamu wengi kama Brazil na Australia zinaongoza mauzo ya bidhaa za Halal kimataifa, ilhali Nigeria haina maandalizi ya kitaasisi kushindana.**

**Anapendekeza mabadiliko ya mitaala kwa hatua tatu: kubadili mtazamo wa Halal kama "kigezo cha ubora", kuchambua minyororo ya thamani yenye faida kubwa, na kufundisha zana za fedha za Kiislamu kama murabaha, sukuk na mudaraba.**

**Anasisitiza kuwa kufungua masoko ya nchi 57 wanachama wa Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Kiislamu (OIC) kunahitaji shule za biashara kubadilika na kuwa vituo vya ubunifu wa Halal.**

**Bila hatua hiyo, anaonya, Nigeria itaendelea "kuagiza kile ambacho ingeweza kusafirisha."**

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




# Mafanikio Sukuk ya Benin yavutia Serikali nchi za nyingine Afrika

Mauzo ya dhamana ya Kiislamu (Sukuk) ya Benin yamevutia viongozi wa nchi nyingine za Afrika na kuangalia fedha zinazokubaliana na Sharia.

Kwa mujibu wa Reuters, Sukuk hiyo, pamoja na mambo mengine, imeonesha fursa ya kupanua vyanzo vya fedha na kuvutia wawekezaji wapya, washauri na wachambuzi wamesema.

Gatien Bon wa Rothschild, ambaye alishauri Benin, alisema Sukuk hiyo imegeuza mtazamo wa wakopaji wa nchi za Afrika. "Hii inaleta utofauti zaidi katika muundo na hivyo katika wigo wa wawekezaji," alisema.

Benin ilitoa sukuk ya miaka saba sambamba na kufungua upya bondi yake ya dola ya mwaka 2038, na kupokea maombi ya zaidi ya dola bilioni 7—yakizidi ukubwa uliopangwa.

Nicole Kearse, mkuu wa fedha za serikali katika African Legal Support Facility (ALSF), alisema wameona "nchi nyingi zikija kuomba mikakati... zikijaribu kuelewa namna hizi zinavyofanya kazi na wahusika wa soko."

Bashar Al-Natoor wa Fitch Ratings alisema utoaji wa sukuk Afrika ulipanda hadi dola bilioni 3 mwaka 2025 kutoka dola milioni 112 mwaka uliotangulia, ukichochewa zaidi na Misri kurudi sokoni kwa dola bilioni 2.8. Kwa 2026 hadi sasa, sukuk zimevuka dola milioni 580, hasa kupitia Sukuk hii ya kwanza ya Benin ya dola milioni 500, Al-Natoor alisema.

Admassu Tadesse, rais wa Trade and Development Bank, alisema kuna "hamu zaidi" kutoka wawekezaji wa Ghuba kufadhili masoko yanayochipukia.

Mohamed Damak wa S&P Global Ratings anatabiri utoaji wa sukuk duniani kufikia dola bilioni 270–280 mwaka 2026, na sukuk endelevu kuendelea kukua.

## Mfumo wa kugawana hatari benki za Kiislamu wasifiwa

**ACCRA, Jan 27 – Taasisi ya Islamic Finance Research Institute of Ghana (IFRI-Ghana) imesema fedha za Kiislamu (non-interest banking) zina mfumo wenye "ulinzi wa hatari" uliojengwa ndani unaowanufaisha wateja na benki, kwa kusisitiza kugawana hatari badala ya kuhamishiana hatari, tofauti na mifumo ya riba.**

**Mkurugenzi Mkuu wa IFRI-Ghana, Dkt. Ali Shaibu, alisema katika mahojiano na 3News kuwa miamala mingi ya fedha za Kiislamu hujengwa kwenye ubia.**

**"Mfumo unatoa bidhaa mbalimbali ikiwemo mudaraba, inayofanana na ufadhili wa mtaji wa ubia (venture capital); benki hutoa mtaji na mteja anaendesha biashara au uwekezaji," alisema.**

**Kwa mujibu wa Dkt. Shaibu, faida hugawanywa kwa makubaliano ya awali baina ya benki na mteja. Aliongeza kuwa endapo hasara itatokea, benki hubeba athari ya kifedha "mradi hasara haijasababishwa na uzembe au utovu wa uadilifu wa mteja," akisisitiza kuwa mpangilio huo huongeza uwazi, usawa na uwajibikaji wa pamoja.**

## Hatua ya kihistoria Algeria ikizindua Sukuk ya kwanza ya Serikali

**ALGIERS – Serikali ya Algeria imefanikiwa kutoa sukuk yake ya kwanza ya serikali yenye thamani ya dinari bilioni 296.65, sawa na takribani dola bilioni 2.3 za Marekani, kwa lengo la kufadhili miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali za kimkakati.**

**Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Fedha, sukuk hiyo ina muda wa miaka saba na inatoa faida ya kudumu ya asilimia sita kwa mwaka. Malipo ya faida yatafanywa kwa mfumo wa kodi (rent), kulingana na misingi ya fedha za Kiislamu, na yatakuwa hayatozwi kodi.**

**Usajili wa sukuk umefunguliwa kwa raia wa Algeria wanaoishi ndani na nje ya nchi, pamoja na taasisi na makampuni yanayoendeshwa chini ya sheria za Algeria, Hazina ya Umma ilisema. Kipindi cha usajili kitaendelea hadi lengo la fedha litakapofikiwa.**

**Sukuk hizo zimehakikishwa kwa mali za umma zisizohamishika, ambazo hutumika kama dhamana chini ya muundo wa sukuk, na zinaweza kuuzwa kati ya wawekezaji au kuorodheshwa kwenye soko la hisa endapo zitahifadhiwa kupitia benki.**

## Pakistan, Malaysia katika ushirikiano halal

**ISLAMABAD/KUALA LUMPUR,– Pakistan na Malaysia zimefanya mazungumzo mapya ya kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi yakilenga chakula cha halal, nishati jadidifu na utalii, hatua inayolenga kupanua biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili zenye Waislamu wengi, kwa mujibu wa taarifa rasmi iliyochapishwa katika tovuti ya Minute Mirror.**

**Katika mazungumzo jijini Kuala Lumpur kati ya balozi wa Pakistan nchini Malaysia, Syed Ahsan Raza Shah, na Gavana wa jimbo la Sarawak, Wan Junaidi Tuanku Jaafar; pande hizo mbili zilipitia ushirikiano uliopo.**

**Pande hizo pia kuchunguza fursa mpya kwenye uzalishaji wa halal, biashara ya mafuta ya mawese, kilimo, ajira, utamaduni na maendeleo endelevu. Biashara ya pande mbili inakadiriwa kuwa karibu dola bilioni 1.4 kwa mwaka.**

# Sura tofauti matokeo kidato cha nne

Baraza la Mitihani Tanzania (Necta) limetangaza matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne uliofanyika Novemba 2025, yakionesha picha mseto ya ufaulu ambapo wasichana wameongoza kwa idadi ya waliofaulu, huku wavulana wakionesha ubora zaidi wa ufaulu kwa madaraja ya juu.

Matokeo hayo yanaonesha kuwa ufaulu umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024, hali inayoashiria maendeleo katika sekta ya elimu licha ya changamoto zinazoendelea kujitokeza katika baadhi ya masomo, hususan sayansi na hisabati.

Akizungumza wakati wa kutangaza matokeo hayo jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa Necta, Profesa Said Mohamed alisema jumla ya watahiniwa 526,620 sawa na asilimia 94.98 wamefaulu kwa kupata daraja la kwanza hadi la nne.

Ufaulu huo ni ongezeko la asilimia 2.61 ikilinganishwa na matokeo ya mtihani wa mwaka 2024 uliokuwa asilimia 92.37.

Profesa Mohamed alisema wasichana walikuwa wengi zaidi miongoni mwa watahiniwa waliofanya mtihani huo. Jumla ya wasichana 295,032 walifanya mtihani wa kidato cha nne, ambapo 278,108 sawa na asilimia 94.26 walifaulu.

Kwa upande wa wavulana, watahiniwa 259,426 walifanya mtihani huo na kati yao 248,512 sawa na asilimia 95.79 walifaulu.

"Tofauti iliyopo ni kwamba ubora wa ufaulu wa madaraja ya kwanza hadi ya tatu umeonekana kuwa mzuri zaidi kwa wavulana, wakati wasichana wakiwa wengi zaidi kwa idadi ya wanaofaulu," alisema Profesa Mohamed.

## Vita ya wavulana wasichana

Katika matokeo hayo, uchambuzi unaonesha waliopata daraja la kwanza wasichana walikuwa 24,455 huku wavulana wakiongoza kwa 31,958.Daraja la pili wasichana 38,772 wavulana 46,224.Daraja la tatu wasichana 56,501 huku wavulana wakiwa 57,494.

Kwa upande wa daraja la nne wasichana ni 158,380 huku wavulana wakiwa 112,836.

Akizungumzia hilo mchambuzi wa elimu Stella Mrema, alisema takwimu hizo zinaonesha tofauti ya kimfumo katika namna wanafunzi wa kike na wa kiume wanavyojiandaa na kushindana kielimu.

"Wasichana wamekuwa na nidhamu nzuri ya kuhudhuria masomo na kumaliza shule, ndiyo maana wanaongoza kwa idadi ya wanaofaulu. Hata hivyo, wavulana wanaonekana kuwekeza zaidi kwenye masomo yanayowapa alama za juu, jambo linalowaweka juu katika ubora wa ufaulu," alisema.

Mtaalamu wa mitalaa, Anna Kweka alisema ufaulu wa asilimia karibu 95 ni mzuri kitaifa, lakini maswali makubwa yako kwenye masomo ya sayansi.

## Ufaulu kimasomo

Profesa Mohamed alisema katika somo la fizikia, ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 32.59 mwaka 2024 hadi asilimia 44.21 mwaka 2025, huku hisabati ikiendelea kuwa na ufaulu wa chini, ambapo ni asilimia 26.45 pekee ya watahiniwa waliofaulu.

Biolojia nayo imeonesha kushuka kwa ubora wa ufaulu kwa asilimia 15.12, huku waliofaulu wakiwa asilimia 65.68.

"Haya ni masomo yanayounda msingi wa sayansi na teknolojia. Kama bado tuna wanafunzi zaidi ya asilimia 70 wanaofeli hisabati, lazima tukubali kuwa tatizo ni la kimfumo," alisema Kweka.

Kwa upande wa masomo ya lugha, wachambuzi walisema matokeo yanatia moyo. Takwimu zinaonesha asilimia 97.82 ya watahiniwa wamefaulu Kiswahili, huku Kiingereza, Kifaransa na Kichina yakifanya vizuri kwa ufaulu wa kati ya asilimia 79.48 hadi 93.43.

Hata hivyo, somo la Kiarabu limeendelea kuwa na ufaulu wa chini licha ya kuongezeka hadi asilimia 50.62 kutoka asilimia 33.86 mwaka 2024.

Masomo ya sayansi ya jamii nayo yameonesha ongezeko la ufaulu, jiografia imeongoza kwa kupanda kwa asilimia 7.55, ikifuatiwa na historia kwa asilimia 4.87.



MWANDISHI WETU

# Mauzo karafuu nje ya nchi yaongezeka kwa 25.1%

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imesema mauzo ya karafuu za Zanzibar nje ya nchi yameongezeka kwa asilimia 25.1. Taarifa ya BoT kuhusu mwenendo wa uchumi kwa mwezi Desemba 2025, inaonesha mauzo hayo yamefikia shilingi bilioni 60.5 (sawa na Dola za Marekani milioni 23.7) ikilinganishwa na kiasi kilichorekodiwa mwaka 2024.

Taarifa hiyo imefafanua kuwa ongezeko hilo la mauzo ya karafuu linatokana na mabadiliko ya uzalishaji unaohusiana na mzunguko wa uvunaji wa karafuu. Aidha, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kwa ujumla yaliongezeka kwa asilimia 30.4 hadi kufikia shilingi trilioni 4.09 ikilinganishwa na kiasi kilichorekodiwa katika mwaka ulioishia Novemba 2024.

"Mapato ya huduma yameendelea kuimarika yakichochewa na ongezeko la mapato ya huduma za utalii kwa asilimia 26.9 na kufikia watalii 908,049 katika mwaka ulioishia Novemba 2025," ilisema taarifa hiyo. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi kufikia mwezi Novemba 2025 mapato ya ndani na misaada yalifikia shilingi bilioni 191.5 sawa na asilimia 99.3 ya lengo, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 178.9 na kiasi kilichobaki kilikua misaada.

Vilevile, mapato yanayotokana na kodi yalifikia shilingi bilioni 155.5 sawa na asilimia 98.8 ya lengo, hali iliyochangiwa zaidi na kuimarika kwa ulipaji kodi na kuongezeka kwa ufanisi wa usimamizi wa kodi huku mapato yasiyo ya kodi yakifikia shilingi bilioni 23.4 sawa na asilimia 116.3 ya lengo.

# Balozi Kombo akutana na EU kuimarisha uhusiano

Serikali ya Tanzania imefanya mazungumzo na viongozi wakuu wa Umoja wa Ulaya (EU) jijini Brussels nchini Ubelgiji, hatua inayotafsiriwa kuwa mwelekeo mpya wa diplomasia.

Katika mazungumzo hayo, ujumbe wa Tanzania ulioongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, ulijadiliana na viongozi wa EU, kuhusu kuimarisha ushirikiano wa kisiasa, kiuchumi na kiusalama.

Hayo yalifanyika jana Balozi Kombo alipokutana na Makamu wa Rais wa Tume ya Ulaya na Mwakilishi Mkuu wa EU katika Sera za Mambo ya Nje na Usalama, Kaja Kallas nchini Ubelgiji. Balozi Kombo alisema kuna umuhimu wa kuimarisha ushirikiano wa vitendo unaojengwa katika misingi ya heshima ya mamlaka ya kitaifa, biashara inayozingatia utawala wa sheria, uwekezaji unaotabirika na mifumo ya ushirikiano inayotekelezeka.

Ujumbe huo, uliomhusisha pia Waziri wa Nchi kutoka Ofisi ya Rais, Profesa Palamagamba Kabudi, ulikutana pia na Kamati ya Kisiasa na Usalama ya EU (PSC), chombo chenye ushawishi mkubwa kinachoundwa na mabalozi wa nchi 27 wanachama wa umoja huo.

Kupitia kikao hicho, Tanzania iliwasilisha msimamo wake moja kwa moja kwa EU, huku ikithibitisha nafasi yake kama mshirika wa kuaminika katika masuala ya amani, usalama na uthabiti wa ukanda wa Afrika Mashariki.

Katika ngazi ya bunge, Waziri Kombo alifanya mazungumzo katika Bunge la Ulaya, ikiwemo kukutana na Makamu wa Rais wa Bunge hilo, Younous Omarjee.

Mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha diplomasia ya kibunge kama nguzo ya uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na EU, hususan katika biashara, utawala bora na uhusiano wa watu kwa watu.

Katika ziara hiyo pia, ujumbe wa Tanzania ulikutana na kufanya mazungumzo na Kamishna wa EU wa Ushirikiano wa Kimataifa, Jozef Síkela.

Katika kikao hicho, Tanzania ilieleza wazi vipaumbele vyake vya ushirikiano unaozalisha ajira, kukuza ujuzi, kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha miundombinu himilivu na mabadiliko ya kiuchumi.



Ujumbe wa Tanzania uliambatana na Balozi Swahiba Mndeme, Mkurugenzi wa Ulaya, Balozi Jestas Abuok Nyamanga, Mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Ulaya na maofisa wengine waandamizi.

Tanzania inafanya ziara hiyo, ukiwa umepita mwezi mmoja tangu Bunge la EU Novemba 29, mwaka jana lisitishe msaada wa Euro milioni 150 (zaidi ya Sh461.53 bilioni), zilizopaswa kuletwa nchini Januari mwaka huu, kupitia mfuko wa NDICI-Global Europe. Hatua hiyo ya Bunge la EU, ilitokana na kile ilichoeleza, kukithiri vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini vinavyohusisha utekaji wa raia, ukandamizwaji wa wanasiasa wa upinzani na kuminywa kwa uhuru wa kuongea.

Hata hivyo, uamuzi wa bunge hilo, ulijibiwa na Serikali ya Tanzania, ikisema haijatendewa haki, kwa kuwa wakati inajadiliwa haikupewa nafasi ya kusikilizwa kwa upande wake.

Tanzania ilisisitiza kwa kuwa ni Taifa huru halipaswi kupangiwa mambo ya kufanya.

شَعْبان

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

# 'Mnaonadi' miili yenu mitandao ya kijamii ni kwa faida ya nani?

Matumizi ya mitandao ya kijamii hususan Whats App, YouTube, Facebook, TikTok na Instagram yameshika kasi hivi sasa huku kukiwa na athari mbili kubwa kwa watumiaji; athari hasi (hasara), na chanya (faida). Matunda ya athari zote mbili – yawe matamu au machungu hayaepukiki kutokana na ukweli kuwa waathirika hawana pakujificha kwa kuwa bado wangali hai kwenye uso wa dunia.

Ni ukweli usio na chembe ya shaka kuwa, wapo watu wanaojifunza mambo mbalimbali ya maana na faida kupitia mitandao ya kijamii. Hata hivyo, ipo changamoto ya baadhi ya watu ambao kwa makusudi wamekuwa hawazingatii suala la maadili.

Wengi katika hawa ni wale wasiofanya upembuzi katika kuchuja na kutazama kile kinachostahiki kutumwa au kusambazwa mitandaoni. Matokeo ya kadhia yamepelekea kuwapo kundi kubwa la wanawake wanaoiga utamaduni wa kimagharibi kiasi cha kutotii amri ya kujihifadhi miili yao kwa vazi la sitara la hijab.

Ni kwa sababu hiyo, Uislamu umeeleza malengo mahsusi ya hijab. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimwambia Mtume (rehema na amani iwe juu yake) pamoja nasi: "Ewe Mtume! Waambie wake zako, na mabinti zako, na wanawake waumini wateremshe shungi zao. Kufanya hivyo kutapelekea haraka wajulikane (kuwa ni watu wa heshima) wasiudhiwe…" [Qur'an, 33: 59].

Aya hii ni hoja na dalili kuwa vazi la hijab ni ngao ya kutakasa nyoyo za waumini wanawake na kuwahifadhi na mambo yanayoweza kuwashawishi wanaume kuingia katika matamanio ya zinaa.

Tofauti ni kwamba, katika zama hizi wanawake ndiyo ambao wamegeuka kuwa vinara wa kupuuzia mipaka ya maadili katika suala la mavazi. Wengi hujikuta wakitumbukia kwenye dimbwi la upigaji picha zinazoonesha maungo yao na kuziweka kwenye mitandao.

Tabia hii ni yenye kujitenga mbali na ile ya wanawake watiifu kwa Allah pamoja na Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake). Kwa kuzingatia unyeti wa suala hili, ipo haja ya ya kuwakumbusha wanawake wa Kiislamu kujiepusha na uovu huu ili kulinda heshima yao na maadili ya dini.

Tunaamini kuna wengi waliojijengea dhana ya kuamini kuwa Uislamu haujawakataza kuweka picha zao mitandaoni. Swali la msingi na muhimu kujiuliza ni je, kuna faida gani kwa mwanamke wa Kiislamu kuweka picha mtandaoni – sawa akiwa amevaa hijab na kuacha sehemu ya uso au kufunika mwili wote?

Hakuna shaka hali hii hufungua mlango wa fitina (vishawishi) katika jamii. Aghalabu tumekuwa tukishuhudia visa vingi vya kuvunjika kwa ndoa huku sababu kuu ikihusishwa na picha za mitandaoni. Mbaya zaidi ni pale baadhi ya wanaume walioonekana kuwa watakasifu wa nyoyo na tabia lakini kutokana na fitina ya mitandao wakajikuta wakiangukia kwenye mtego wa zinaa.

Kwa hali yoyote ile, haya ni matokeo ya kile kinachoaminika kuwa uzuri na fitina ya mwanamke hupatikana katika sura. Katika kulizungumzia hili, Al–Haafiz Ibn Hajar (Allah amrehemu) amesema: "Utamaduni wa wanawake katika zama zilizopita na za sasa ni kufunika nyuso zao mbele ya mwanaume asiye mahrimu." [Fat–hul Bari, juz. 9, uk. 424].

Tunaamini kufahamika kwa haya ndiyo kupatikana jawabu la uharamu wa mwanamke kuweka picha sehemu ambayo itaonekanwa na watu wema au waovu. Pamoja na hayo, si jambo rahisi kwetu kuiondoa hali hii pasipo kuwalingania wanawake wa Kiislamu kusoma dini yao.

Kama Mtume na Masahaba zake walivyoupigania Uislamu, nasi hatupaswi kusalimu amri katika hili. Licha ya kwamba ni muhali kwa mtu kuiepuka mitandao ya kijamii katika zama hizi, bado ni jukumu letu kuielimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya mitandao.

Hali kadhalika, wanawake wa Kiislamu wanapaswa kutumia mitandao kwa ajili ya manufaa ya dini yao, na siyo kufurahisha nafsi. Si ndoto za alinacha kuwa haiwezekani kutumia mitandao kwa mambo yenye faida katika dini na dunia.

Jambo muhimu la kuzingatia kwa mwanamke wa Kiislamu, ni kujiheshimu kwa kujiepusha kufanya mambo yote yaliyoharamishwa ili apate kufaulu duniani na kesho Akhera. Ikiwa yupo mwenye kutaka kinyume cha haya, basi huyo ndiye arukae mipaka.

Allah anasema katika Qur'an: "Hakika wamefaulu waumini. Ambao ni wanyenyekevu katika swala zao. Na ambao wanajiepusha na (maneno na vitendo vya) upuuzi. Na ambao wanatoa zaka. Na ambao wanazihifadhi tupu zao." [Qur'an, 23:1–5].

شَعْبان

KALAMU HURU

SEHEMU YA 1

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Upunjaji mizani: jinai inayohalalishwa kimyakimya katika jamii zetu

**Tatfif: Dhambi ndogo kwa macho ya watu, kubwa sana kwa mizani ya Allah**

Katika jamii nyingi leo, upunjaji hauonekani tena kama jinai, bali kama ujanja wa kuishi. Hujisitiri kwa majina mepesi kama "kawaida ya kazi", "mbinu za maisha" au "kila mtu anafanya".

Lakini Qur'an inapozungumzia dhambi ya upunjaji mizani (Tatfif), haitumii lugha laini wala onyo la kawaida. Badala yake, inaanza kwa neno zito linalotikisa dhamira na akili ya msomaji: "Ole wao wapunjao."

Aya ya kwanza hadi ya sita ya Sura ya 83, Al-Mutwaffifin, zinaweka wazi hukumu hii kali: "Ole wao wapunjao. Ambao wanapojipimia kwa watu hudai watimiziwe. Na wao wanapowapimia watu hupunguza. Je, hawafikiri kwamba watafufuliwa, katika siku iliyo kuu mno, siku watakaposimama watu mbele ya Mola Mlezi wa walimwengu wote?"

Hili si onyo la sokoni pekee. Ni tamko la kimsingi dhidi ya mfumo mzima wa maisha unaojengwa juu ya dhulma, hila na ubinafsi.

## Mizani ni mfano, sio kikomo

Wengi wanaposoma aya hizi, fikra zao hukwama kwenye kilo ya unga au lita ya mafuta. Hata hivyo, wanazuoni wa tafsiri wamefafanua kuwa kipimo na mizani vilivyotajwa ni mifano, si mipaka ya maana.

Kwa mantiki hiyo kila haki inayodaiwa kikamilifu lakini haitekelezwi kikamilifu, kila mkataba unaotakiwa uzingatiwe kwa upande mmoja lakini upande mwingine unaukwepa, na kila mshahara unaochukuliwa bila kazi kutekelezwa ipasavyo.

Vyote hivyo vinaingia chini ya dhana ya 'Tatfif', hata kama mhusika hajawahi kushika mizani mkononi.

## Qur'an na msingi wa viwango vya uadilifu

Leo mataifa yanajivunia yanajivunia taasisi za viwango na udhibiti zikibatizwa majina mazuri mazuri ikiwemo bureau of standards (taasisi za viwango), quality control (wadhibiti wa ubora) na regulatory authorities (mamlaka za udhibiti).

Kimataifa kuna ISO, shirika la kimataifa, lisilo la kiserikali, ambalo linatengeneza na kuchapisha viwango vya kimataifa kwa ajili ya bidhaa, huduma, na mifumo mbalimbali. Lengo la ISO ni kuhakikisha bidhaa na huduma hizo ni salama (Hazina madhara kwa watumiaji), za kuaminika (zinafanya kazi kama inavyotarajiwa) na zenye ubora zimetengenezwa vizuri na zinakidhi mahitaji.

Lakini ukweli ni kwamba Qur'an ndiyo iliyoweka msingi wa kwanza wa falsafa ya viwango vya uadilifu. Aya hizi zinaweka kanuni kuu tatu zisizobadilika: Kwanza, usijipatie haki kamili kwa kudhulumu wengine, kila haki ina wajibu unaolingana na kila upungufu una hesabu yake.

Tofauti ni kwamba taasisi za dunia huadhibu kwa faini au kufungia shughuli, ilhali Qur'an inaonya kwa Wayl—adhabu nzito ya Akhera.

## Tatfif, kama ugonjwa wa nafsi

Upunjaji mizani hauanzi kwenye mizani, unaanzia kwenye nafsi. Mizizi yake ni tamaa, ubahili, kujiona bora na kumsahau Allah na Akhera. Hii ndio sababu Qur'an inauliza swali la kuumiza dhamira: "Je, hawajui kwa yakini kuwa watafufuliwa?"

Kwa maana nyingine, lau kumbukumbu ya kusimama mbele ya Allah ingekuwa hai mioyoni mwao, wasingethubutu kupunja, hata kwa kiwango kidogo.

## Tatfif ndani ya nyumba

Qur'an haizungumzii wafanyabiashara pekee. Tatfif inaingia hadi ndani ya familia. Mume au mke anayedai haki zote lakini hatekelezi wajibu wake; mzazi anayewataka watoto watii na wajitume, ilhali yeye ni mzembe katika haki zao—wote hawa wanaingia chini ya maonyo haya.

Kwa maana hiyo, tatfif, huharibu familia, huvunja mahusiano, na huondoa baraka katika maisha.

## Hatari ya kuizoea dhulma ndogo

Tatfif mara nyingi huanza kwa kile kinachoonekana kuwa kidogo: dakika chache za uzembe kazini, kazi ndogo kuachwa bila kufanywa, au ubora kupunguzwa kidogo. Vitu vidogovidogo tu.

Lakini Qur'an inatufundisha kwamba dhulma ndogo ikizoezwa hugeuka mfumo, na mfumo huo huangusha jamii nzima na hata taifa bila kelele.

## Hitimisho

Aya za mwanzo za Al-Mutwaffifin zinatukumbusha kuwa mizani haipo sokoni pekee. Ipo ofisini, darasani, hospitalini, maofisini, nyumbani, na ndani ya dhamira za kila mmoja wetu.



# شَعْبان فتاوى



**SHEIKH**
Shaaban Mussa
0786 272 323

## Swali: Ni ipi hukumu na masharti ya kumuasili mtoto?

**Jibu:** Neno kuasili lina maana mbili kuu: Mosi, kumpa mtoto ambaye si wako kisheria haki ya ubini; kumtambulisha kana kwamba ni mwanao halisi na kumthibitishia haki zote zinazomhusisha mtoto wa damu.

Pili, kuasili pia ni kumlea mtoto ambaye si wako wa nasaba; kumtunza, kumuelimisha, kumpa upendo, ukarimu na usalama, kumlinda asiharibike au kupotea kutokana na kufiwa, umaskini wa wazazi wake, au kutimiza utashi wa kimaumbile pale wazazi/walezi wake hawana mtoto wa kumzaa.

Kuhusu kumuasili mtoto kwa kumtambulisha na ubini wako au ukoo wako si halali kisheria. Kwenye Qur'an, Sura al-Ahzab [33:4-5], Allah anasema: "Wala Allah hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa wanenu. Hayo ni maneno ya vinywa vyenu tu. Na Allah ndiye anayesema kweli. Waiteni (watoto wa kupanga) kwa majina ya baba zao, maana huo ndio uadilifu zaidi mbele ya Allah. Na iwapo hamuwajui baba zao, basi watambueni kama ndugu zenu katika dini, na rafiki zenu, wala si lawama kwenu kutokana na makosa yenu. Allah ni Mwenye kusamehe na Mwenye rehema."

Kwa upande mwingine, hakuna pingamizi la kisharia kumhurumia mtoto huyo, kumlea kwa wema, na hata kumgawia mali kwa sharti mali hiyo itolewe kwa hiari na kwa uwazi, pasipo kumhusisha kisheria na ubini wako au ukoo wako.

Kwa vitendo, ikiwa utampata mtoto wa kumlea, mlee kwa sababu za utu lakini mnasibishe kwa ubini wa baba yake mzazi kama unamjua, na iwapo hamjui mwite kwa jina la kimsingi kama bin Abdallah, bin AbduRahman, n.k.

*Sababu ya tahadhari hii*

Mosi, kumnasibisha mtoto kwa ubini wako bila uhusiano wa kweli kunaweza kusababisha migongano ya kisheria, kudanganya familia, au matatizo ya mirathi. Pili, kuna hatari ya kumuingiza kwenye michaganyiko ya kifamilia isiyo halali kwake na kwa familia.

Kifupi, kumuasili mtoto kwa ubini au ukoo usiomhusu ni haramu kisheria kwa mujibu wa Qur'an.

Na kwa Muislamu, Qur'an ndio chanzo cha kwanza cha maamuzi ya kisheria, na Sunna inasisitiza kuwa kumuasili mtoto kwa ubini wako bila uhusiano wa kweli ni dhambi kubwa. Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Kuna mwanamke amefiwa na mume, na huyo mume wake hakuwahi kumkabidhi mahari wala kumuingilia, je, ana haki ya mahari ya mfano (Mahr al-Mithl), au nusu ya mahari ya mfano au nafaka ya faraja (Mut'ah)?

**Jibu:** Mwanamke ambaye mume wake amefariki kabla ya kumkabidhi mahari na bila kujamiiana naye, ana haki ya mahari ya mfano (Mahr al-Mithl), kama ilivyothibitishwa na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Hadith inaeleza kwamba kuna mtu aliuliza kuhusu kesi kama hii, na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliagiza kwamba mwanamke huyo apewe mahari sawa na ya wake wengine katika jamii yake, bila ukatili au mzaha.

Na Mwanamke anapaswa akae eda (muda wa kusubiri baada ya kifo cha mume) na ana haki ya urithi.

Hadith ya Ma'qil bin Sinan al-Ash'ariy inaonesha mfano wa mwanamke aitwaye Bi'r-wa' bint Washiq, ambaye mume wake alifariki, na hakuwahi kumkabidhi mahari yake, na wala hakuwahi kumuingilia. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alihukumu apewe mahari ya mfano kwa kulinganisha na mahari walizolipwa wake wengine, na pia alimruhusu urithi, huku akimtaka akae eda ya kufiwa na mume.

Kifupi, hukumu hii inamhusu mume ambaye ameoa mke na kabla hajamuingilia amefariki pasipo kuafikiana naye mahari maalum.

Mwanamke haachwi bila mahari, maadili na Sheria ya Kislamu yanahitaji kumpatia mahari ya mfano hata kama marehemu hakuwahi kuingia naye faragha.

Onyo: Kutozingatia utaratibu huu ni makosa, huharibu heshima ya ndoa, huleta dhuluma ya haki ya mke, na hivyo ni jukumu la jamii kuzizuia tabia za hovyo kama hizi. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

شَعْبان

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

# Katika ubunifu, AI si mbadala wa fikra za mwanadamu




Katika zama za sasa za teknolojia, akili bandia (AI) imekuwa kama jibu la haraka kwa karibu kila swali. Kuandika, kupanga, kuchambua, hata kubuni mawazo mapya—watu wengi wanageukia AI kwa matumaini ya kupata suluhisho la haraka.

Hata hivyo, utafiti na majaribio ya kitaaluma yanaonyesha kuwa linapokuja suala la ubunifu wa kweli, binadamu bado ana nafasi ya kipekee ambayo mashine haiwezi kuichukua.

Makala iliyoandikwa na Jesús Escudero, ikitegemea tafiti na majaribio ya Profesa Brian Uzzi wa Chuo cha Kellogg, inaeleza kwa kina kwa nini kutegemea AI katika ubunifu kunaweza kupunguza badala ya kuongeza ubora wa mawazo.

Makala hiyo, When It Comes to Creativity, AI Doesn't Always Have the Answer, inaonyesha kuwa AI ina nguvu katika kasi na ufanisi, lakini ina mipaka mikubwa katika kutoa mawazo ya kipekee na yasiyotabirika.

Ili kuwathibitishia wanafunzi wake, Profesa Uzzi alifanya jaribio darasani akitumia kipimo kinachoitwa Divergent Aptitude Test (DAT), ambacho hupima ubunifu wa jumla, akilinganisha mwanadamu na roboti. Majibu yalionesha kuwa wastani wa wanafunzi ulilingana karibu kabisa na wa roboti, na baadhi ya wanafunzi waliibuka na majibu ya ubunifu wa juu zaidi kuliko AI.

Hata hivyo, Uzzi aligundua kuwa hata baada ya wanafunzi kuona kuwa roboti haikuwa mbunifu zaidi yao, bado walipendelea majibu yake kwa sababu yalikuwa ya haraka. Lakini ubunifu haupimwi kwa nani amemaliza kwanza, bali kwa nani ametofautiana zaidi. Ubunifu wa kweli unahitaji mchakato—kuuliza maswali sahihi, kuchunguza, kukosea, na kujenga mawazo hatua kwa hatua.

Uzzi anapendekeza mfumo wa kuangalia AI kama mshirika, si mbadala. Anaeleza ngazi tatu za matumizi ya AI: uotomatiki (automation), majibu (answers), na ushirikiano (alliances). Anasema kilele cha matumizi ya AI ni ubunifu, mkakati, na uvumbuzi, ambako mchango wa binadamu hauwezi kubadilishwa.

Kwa ujumla, makala ya Jesús Escudero inaweka ujumbe muhimu: ubunifu ni shughuli ya kibinadamu kwa asili. Hutokana na uzoefu, mijadala, na ushirikiano wa watu. AI inaweza kusaidia kupanua fikra, lakini ikitumika vibaya inaweza kuzipunguza. Katika dunia inayokimbilia majibu ya haraka, changamoto kubwa ni kukumbuka thamani ya mchakato wa kufikiri polepole na kwa kina.

NA MWANDISHI WETU

# Wamarekani waandamana kupinga sera za Trump dhidi ya Waislamu



Maelfu ya waandamanaji wamejitokeza katika miji mbalimbali nchini Marekani kupinga sera kali za Rais wa Marekani, Donald Trump na kauli tata zake za kudhalilisha jamii za wachache, hususan Waislamu.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Anadolu Ajensi, kipekee waandamanaji hao wanadai kusitishwa kwa operesheni za Idara ya Uhamiaji na Forodha (ICE) kuwafurusha wageni: Waislamu na makundi mengine yaliyotengwa.

Jiji la Los Angeles limekuwa kitovu cha maandamano hayo, huku maelfu wakikusanyika barabarani kuonyesha hasira na hofu yao dhidi ya kile wanachokieleza kama matumizi ya nguvu kupita kiasi zinazotumiwa na ICE.

Maandamano hayo yamechochewa zaidi na vifo vya raia wawili wa Marekani, Renee Good na Alex Pretti, waliodaiwa kuuawa na maafisa wa ICE katika jimbo la Minnesota, tukio lililoibua maswali mapya kuhusu uwajibikaji wa vyombo vya dola.

Takwimu kutoka mashirika ya haki za binadamu zinaonesha kuwa tangu mwaka 2017, zaidi ya wahamiaji milioni 1.5 wamekamatwa na ICE, huku zaidi ya 250,000 wakifukuzwa kila mwaka, wengi wao kutoka nchi zenye idadi kubwa ya Waislamu na jamii maskini. Waandamanaji wanasema sera hizi zinakiuka haki za binadamu na kuchochea hofu, ubaguzi na kuvunjwa kwa familia, hasa katika majimbo yanayoongozwa na chama cha Democratic kama California.

Huko Los Angeles, maandamano yaligeuka makabiliano ya waandamanaji na polisi na kulazimisha polisi kutumia dawa ya kutoa machozi. Polisi jijini humo wametangaza mkusanyiko huo kuwa haramu huku majengo ya serikali yakifungwa kwa hofu ya usalama.

Viongozi kadhaa, wakiwemo wabunge na madiwani, wameungana na waandamanaji, wakimkosoa Trump na kutoa wito wa mageuzi ya sera za uhamiaji na kutaka sauti za wananchi waliokimbia vita na mateso kusikilizwa kwao badala ya kukandamizwa kwa nguvu.

Maandamano na migomo mikubwa pia yaliripotiwa California, Oregon, Minessota na kwingineko.

## Wanawake wa Kiislamu waendelea kukumbana na unyanyasaji Ulaya

**Maelfu ya waandamanaji walikusanyika Uwanja wa Vredenburg, Utrecht, nchini Uholanzi, kulaani ukandamizaji na ubaguzi wa kimfumo dhidi ya Waislamu barani Ulaya, kufuatia tukio lililorekodiwa kwa video likimuonesha askari akiwashambulia wanawake wawili Waislamu.**

**Tukio hilo limezua hasira ya umma na mjadala kuhusu chuki za muda mrefu dhidi ya Uislamu ndani ya vyombo vya dola, limeripoti shirika la Anadolu Agency.**

**Katika video hiyo, askari anaonekana akimpiga mmoja wa wanawake kwa rungu na kumkanyaga mwenzake tumboni, kitendo kilichotafsiriwa na waandamanaji kama matumizi mabaya ya nguvu na ubaguzi wa wazi.**

**Mashuhuda walisema tukio hilo si la kipekee, bali ni sehemu ya mtiririko wa visa vinavyolenga Waislamu, hususan wanawake wanaovaa hijabu, katika maeneo ya umma.**

**Waandamanaji wanadai haki kwa waathirika hao wakitoa wito kwa mamlaka za Uholanzi kuomba radhi hadharani, kumsimamisha kazi askari aliyedaiwa kuhusika, na kuchukua hatua za kisheria kuzuia vitendo kama hivyo.**

**Wakipiga kelele za "No justice, no peace," (hakuna haki, hakuna amani) na "Hapana kwa polisi wabaguzi," umati huo uliandamana hadi kituo cha polisi cha Paardenveld, ukisisitiza uwajibikaji na mageuzi ya kweli ndani ya vyombo vya usalama.**

**Polisi wa Uholanzi wamethibitisha kuanzishwa kwa uchunguzi rasmi, wakisema picha na video zote zitachunguzwa kwa kina. Hata hivyo, waliongeza kuwa mmoja wa wanawake amekamatwa kwa tuhuma za kumtukana askari, tamko lililozua maswali mapya kuhusu mizani ya haki na ulinzi wa waathirika.**

**Wakili wa wanawake hao amedai askari alitoa kauli za kibaguzi wakati wa tukio, na kuthibitisha kuwa waathirika wote wawili walipata majeraha na wanaendelea kupata matibabu.**

**Shirika la Haki za Msingi la Umoja wa Ulaya (FRA) linasema zaidi ya asilimia 50 ya Waislamu**

**MAKALA MAALUM**

Na Said Rajab
0783 650 803

# Ujumbe wa kukaribisha mwezi Mtukufu wa Ramadhan

**Ndugu zangu katika imani, tunauanza mwezi Mtukufu wa Ramadhan ndani ya siku chache zijazo 'Insha Allah'. Mada yangu leo ni ukumbusho mfupi kuhusu mwezi huu wa ajabu. Kwanini tunafunga? Nini tunatarajia kupata kutokana na kufunga? Na vipi tunaweza kuifanya Ramadhan kuwa bora zaidi kwetu?**



# Ujumbe wa kukaribisha mwezi Mtukufu wa Ramadhan

Nini tunapaswa kufanya ili kupata fadhila za Ramadhan? "Enyi mliyoamini! Mmeamrishwa swaumu (kufunga), kama walivyoamrishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumchamungu." [Qur'an, 2:183]. Wale miongoni mwetu tunaofunga, tunafurahia na kuridhika kwamba tunaacha vyakula na vinywaji vyetu vitamu, starehe na burudani zetu halali ili tu kumpendeza Mola wetu.

Mwenyezi Mungu anatuambia ndani ya Kitabu chake Kitukufu majukumu yetu yote kuhusu masikini, wenye kuhitaji, familia zetu na sisi wenyewe, lakini kufunga swaumu amesema ni kwa ajili yake tu, naye humlipa amtakaye. Lazima tukumbuke kila wakati kusudio la kufunga kwetu. Siyo tu kushinda na njaa au kiu, bali ni kuwa hadhiri na Mwenyezi Mungu wakati wote.

Kufunga kunatufundisha kudhibiti matamanio na tamaa zetu za mwili. Tamaa hizo mara nyinyi hutuvuta kwenye matendo yote ya chuki, aibu, wivu, uchoyo, zinaa, hasira na visasi. Kufunga hutusaidia kuwa na nidhamu na kuimarisha dhamiri yetu. Yaani kudhibiti matamanio na tamaa zetu za mwili, ili mawazo yetu, maneno yetu na matendo yetu yawe mema yenye kumpendeza Mwenyezi Mungu.

Ndugu zangu katika imani, tutumie mwezi wa Ramadhan kama fursa ya kufanya jitihada ya kudhibiti tamaa na matamanio yetu ya mwili ili kujenga nidhamu ya kudumu, siyo tu kwa ajili ya Ramadhan hii bali maisha yetu yote. Bila shaka shetani atatujaribu kila mara na kuyafanya maovu yaonekane yenye kupendeza machoni mwetu.

Lakini lazima tuwe macho, na lazima tuyakumbuke yale yanayompendeza Mwenyezi Mungu. Lazima tuseme "Audhubillah mina shaytwanir rajim" (Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na shetani aliyelaaniwa). Lazima tukumbuke kila mara kwamba Mwenyezi Mungu atatuhesabu kwa matendo yetu.

Hatutakiwi kuwa miongoni mwa wale waliopotea, ambao mwisho wao ni Moto wa Jahannam. Tunatakiwa kuwa miongoni mwa waliofuzu, wale watakaoingia Peponi 'Insha Allah!' Tunatakiwa kutumia maisha yetu kwa kutakasa mawazo, maneno na matendo yetu ili tutakapokufa tuwe na moyo na roho iliyotakaswa. Tunatakiwa roho zetu ziwe safi na zisiwe na dosari kama siku tuliyozaliwa.

Aya za mwisho za Surat Al–Fajr, kwa kweli ni maneno ambayo sote tungependa kusikia kutoka kwa Mwenyezi Mungu, wakati tunapokufa na kurejea kwake: "Ewe nafsi iliyotua! Rejea kwa Mola wako ukiwa umeridhika, na umemridhisha. Basi ingia miongoni mwa waja wangu, Na ingia katika Pepo yangu." [Qur'an, 89:27–30].

Mwezi wa Ramadhan ni wakati wetu wa kuwakumbuka ndugu zetu wanaofunga kila siku ya maisha yao, si kwa kupenda, si kwa sababu wanataka kufunga, bali kwa sababu ya umasikini. Hawana chakula cha kutosha wala maji ya kunywa. Sisi tunaofurahia maji safi ya kunywa, milo mitamu kila siku na nyumba za kifahari, lazima tukumbuke kwamba tuna bahati sana kupata baraka hizi.

Mwezi wa Ramadhan, pia ni wakati wa kuonesha huruma na rehema kwa wasiojiweza. Unajua, kila wakati Muislamu anapoanza kitendo muhimu husema "Bismillahi Rahmani Rahim", yaani naanza kitendo hiki kwa "Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Huruma!"

Ndugu zangu katika imani, ni mara ngapi kwa siku tunatamka maneno haya? Hakika ni maneno yenye athari fulani kwenye tabia zetu, ikiwa kweli tunafahamu maana yake. Huruma na rehema lazima vigeuke kutoka maneno matupu na kuwa vitendo vyetu vya kila siku.


Tabia zetu ziendane na rehema na huruma ya Mwenyezi Mungu. Hili ni moja ya mafunzo makubwa ya Ramadhan. Ndiyo maana ni muhimu kwetu kutoa zaka katika mwezi wa Ramadhan. Zaka ni asilimia 2.5 ya mali isiyotumika, inayowaendea masikini na wenye kuhitaji. Tujaribu kukumbuka mafunzo haya muhimu ya Ramadhan.

Wengi wetu hudhani mwezi Mtukufu wa Ramadhan ni wakati wa kuwa goigoi na kuepuka kujituma. Baadhi yetu, kama wangekuwa na fursa, wangependa kulala siku nzima hadi muda wa kufuturu. Hayo ni makosa makubwa! Ramadhan si wakati wa kulala usingizi kama pono! Hayo si maagizo ya Uislamu! Ramadhan ni wakati ambao tunapaswa kujipinda katika ibada, kusoma na kuielewa Qur'an, kujifunza dini yetu na kujaribu kuboresha maarifa na tabia zetu.

Matukio mengi mazito katika historia ya Uislamu yamefanyika ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Qur'an ilifunuliwa ndani ya mwezi wa Ramadhan. Vita vya Badri vilipiganwa ndani ya mwezi wa Ramadhan.

Makka ilikombolewa na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) bila ya kumwaga damu, ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Tariq bin Ziyad alitwaa Uhispania ndani ya mwezi wa Ramadhan, na orodha ni ndefu.

Kwa hiyo, kumbuka Ramadhan si kisingizio cha uvivu na uzembe. Ni wakati wa kujiboresha, kuimarisha akili, mwili na roho zetu. Lazima tuikaribishe Ramadhan kama rafiki aliyepotea kwa muda mrefu.



شَعْبان

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 2 NA YA MWISHO

Na Said Rajab
0783 650 803

# Maana ya haki katika mtazamo wa Kiislamu

**Katika toleo lililopita tulimalizia kwa kuonesha msimamo wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) kuhusu haki, aliposema: "Wallahi, lau Fatimah, binti wa Muhammad angeiba ningeliukata mkono wake." [Sahih Bukhari].**

**Tulisema, kitendo hiki hakikuwa cha kinyama, bali ulikuwa ni usimamizi wa kanuni. Haki lazima itendeke kwa usawa bila ya kujali wewe ni nani. Hakuna upendeleo maalumu (special treatment) mbele ya sheria ya Mwenyezi Mungu. Haki inaonekanaje katika maisha ya kila siku?**

**Hauhitaji chumba cha mahakama ili kutenda haki, bali kinachohitajika ni dhamira tu. Haki inaonekana hata katika jinsi unavyowaadhibu watoto wako. Je, unatenda kwa haki, au kwa sababu ya kuchanganyikiwa? Unaposuluhisha migogoro ya kifamilia, je huegemei upande wowote. Au unaongozwa na hisia au mihemko? Unavyoshiriki mtandaoni, je unaangalia vizuri kile unachochapisha au unaeneza madhara?**

**Leo tumalizie sehemu iliyobaki ya makala haya kwa kuangalia kanuni za Kiislamu zitakazosaidia kuishi kwa haki zaidi katika ngazi ya familia, jamii, taifa na dunia kwa ujumla.**

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Ni uongo wa kutosha kwa mtu kusema kila kitu anachosikia." [Sunan Abi Daudi hadith namba 4992]. Hata katika kuzungumza na kukaa kimya, haki inahitajika. Pengine tujiulize, haki katika ulimwengu wa leo, jukumu letu ni lipi kama Waislamu? Wakati tunaposhuhudia mauaji kule Gaza, Sudan, Iraq, Syria, Libya na kwengineko, imani yetu inatutaka tufanye nini?

Kwanza ni kutohalalisha ukandamizaji bila kujali mkandamizaji ni nani, pili kusema ukweli hata kama haupendwi, na tatu kusimama na wanaokandamizwa, si kwa sababu ya siasa za utambulisho bali kwa sababu ya wajibu wa kiungu.

Allah 'Azza Wajallah' anasema: "Wala msiwategemee wanaodhulumu, usije ukakuguseni Moto..." [Qur'an, 11:113]. Kunyamazia dhuluma – iwe kwenye nyumba zetu au ulimwenguni kote, hakuna maana ya kutoegemea upande wowote bali ni kushiriki kufanya dhuluma hiyo.

## Haki inaanzia nyumbani

Kabla hatujaanza kuipigia kelele serikali au taasisi kwa ukosefu wa haki, tunahitaji kujichunguza wenyewe kwanza. Je, tunatenda haki kwa wenza wetu na watoto?

Je, tunafanya usawa kwa ndugu zetu katika urithi au mapenzi? Je, tunafanya biashara zetu kwa haki bila udanganyifu au unyonyaji? Je, tunatekeleza haki ya kihisia bila kupuuza hisia za wengine? Umar bin Khattwab (Allah amridhie) alipata kusema: "Jiwajibishe mwenyewe kabla hujawajibishwa." Na haki halisi huanza na uaminifu.

## Kanuni za kuishi katika haki

Zifuatazo ni kanuni za Kiislamu zitakazokusaidia kuishi kwa haki zaidi. Mosi, angalia nia yako kwa sababu haki huanzia moyoni; pili, utakase moyo wako kutokana na ubinafsi, chuki, au maslahi binafsi; na tatu jielimishe kuhusu jinsi dhuluma inavyoonekana, kuanzia ubaguzi wa rangi, unyonyaji wa kiuchumi, hadi upendeleo wa kijinsia.


Kanuni ya nne ni kusema ukweli kwa hekima – siyo lazima upayuke ili uwe muadilifu bali kuwa mkweli na mwenye msimamo. Fanya mambo kwa haki, hata kama hakuna anayekuona, kwani uadilifu ni kutenda haki faraghani.

Usichukue njia za mkato, hata katika mambo unayodhani ni madogo. Muombe Allah 'Azza Wajallah' akupe moyo mwema na uongofu kwa sababu haki siyo tu ni 'legal' (jambo la kisheria) bali ni jambo la ndani kabisa kiroho.

Haki siyo jambo tunalokimbilia kwa sababu ni rahisi, au tunalopuuza kwa sababu ni gumu, bali ni amana tukufu kati yetu wenyewe kwa wenyewe na kati yetu na Mwenyezi Mungu. Allah anasema: "Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu na dalili zilizo wazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na mizani (ya mema na maovu), ili watu wasimamie haki na uadilifu..." [Qur'an, 57:25].

Qur'an Tukufu, Mtume Muhammad, na ujumbe mzima wa Uislamu, vyote hivyo vinalenga jambo moja kubwa; nalo ni kujenga jamii yenye haki iliyojikita kwenye rehema, ukweli na uwajibikaji. Haki siyo maamuzi binafsi, ni Uislamu kwa vitendo.

Mwenyezi Mungu atufanye kuwa wenye kutenda haki katika nyumba zetu, kazini na ulimwenguni kote, na asitufanye kuwa miongoni mwa wale wanaofumbia macho dhuluma, bali miongoni mwa wale wanaosimama kidete katika haki na ukweli bila kujali gharama zake.



شَعْبان

MAKALA MAALUM

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA



SEHEMU YA 2

# Fursa za kuchuma mali katika kipato halali

**Haifichiki kwa mtu mwenye akili timamu kuwa, sharia ya Allah imekuja kulinda na kutimiza maslahi ya waja, kuwalinda na maafa, ufisadi, na kuvunjika kwa mpangilio wa jamii. Wanazuoni wa Kiislamu wamekubaliana kuwa, kulinda mali, kwa ujumla wake ni miongoni mwa misingi mikuu ya sharia.**

**Ama suala la kutafuta mali, kuikuza na kuitumia, hilo liko katika kiwango cha mahitaji muhimu (ḥajiyyaat) yanayopewa nafasi inayokaribia daraja la dharura. Kwa sababu hiyo, kuzungumzia njia na mipaka ya kipato halali katika Uislamu si jambo la ziada au la pembeni, bali ni miongoni mwa wajibu muhimu unaopaswa kupewa uzito unaostahiki.**

Hakika kutafuta kipato cha halali ni katika wajibu mkubwa kabisa, kama alivyosema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Kutafuta riziki ya halali ni wajibu juu ya kila Muislamu", hasa katika zama hizi ambazo watu wengi hawajali tena iwapo wanachokipata ni cha halali au haramu.

Mtume alibashiri hali hii kwa kusema: "Zitafika zama ambazo mtu hatojali anachokipata kama ni cha halali au cha haramu." Athari ya kula haramu hujitokeza katika mienendo na tabia ya mtu na hatimaye huathiri viungo vyake vyote. Kwa sababu hiyo, ni bora kwa muumini kipato chake kiwe cha halali kuliko kuomba watu au kujipatia kipato cha haramu.

Mtume amesema: "Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake. Mmoja wenu kuchukua kamba yake akaenda mlimani kukata kuni kisha akazibeba mgongoni mwake na akala (kwa kipato hicho); hilo ni bora kwake kuliko kuwaomba watu, na ni bora kwake kuliko kula haramu." Zaidi ni kwamba, anayekula haramu hufungiwa milango ya mbinguni.

Mtume alitaja habari ya mtu anayesafiri muda mrefu, mwenye nywele timtim na zilizochafuka na vumbi, anainua mikono yake mbinguni akiomba: "Ewe Mola wangu! Ewe Mola wangu!" ilhali chakula chake ni cha haramu, kinywaji chake cha haramu, mavazi yake ya haramu, na amekuzwa kwa (kipato) haramu; basi vipi dua yake itakubaliwa mtu huyo?"

Uislamu umeipa mali uangalizi wa pekee na kuwa miongoni mwa mahitaji ya lazima ya maisha. Mara nyingi Qur'an imeunganisha kutajwa kwa mali, nafsi pamoja na watoto ili kubainisha hadhi yake, kusisitiza umuhimu wake, na kuthibitisha kuwa Uislamu ni dini ya maisha.

Mali ni nguzo ya kusimama kwa dini na ni sababu ya kuendelea kwa maisha. Mali ni uti wa mgongo wa maisha, na kupitia mali maslahi ya watu, ustawi wao, na mahitaji yao huparikana. Vilevile mali ni pambo la maisha ya dunia.

Mtu anapokuwa fakiri hudharauliwa na wengine, na dunia humbana licha ya upana wake. Vivyo hivyo, hazina za taifa katika nchi zinapokauka, hadhi ya nchi hiyo huporomoka, adui huidharau, nchi hushindwa kujilinda na kuwa huru kimaamuzi.

Pia, mali ni mtihani na majaribu. Wapo wanaofanikiwa na kuokoka kupitia mali zao, na wapo wanaoharibika na kuangamia kwa sababu ya kumiliki mali. Kwa sababu hiyo, sharia ya Kiislamu imeeleza kwa kina njia halali za kupata mali, namna ya kuizungusha na kuiwekeza, jinsi ya kuitumia na kunufaika nayo, na imeweka mipaka na kanuni zinazoainisha yaliyo halali na yaliyo haramu.

Pamoja na hadhi na umuhimu wake wote, mali hubaki kuwa njia, si lengo. Lengo lake ni kusimamisha maisha, kutimiza mahitaji, na kutekeleza wajibu. Allah anasema: "Na utafute kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu makazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi." [Qur'an, 28:77].

Na Mtume (rehema na amani zimshukie) alimwambia Amr bin al–Aṣ (Allah amridhie): "Ewe Amr! Mali iliyo bora ni ile inayomilikiwa na mtu mwema." Iwapo mali itageuzwa kuwa lengo la maisha na kumshughulisha mwanadamu mpaka akasahau au akapuuza yale yaliyofaradhishwa na Allah, basi hapo mali hubadilika na kuwa mzigo mzito, fitina, na chanzo cha maangamizi kwa mwenyewe.


Katika hali hiyo, mali huwa sababu ya hasara, kuporomoka, na maangamizi, badala ya kuwa chombo cha kheri na ujenzi wa maisha. Allah anasema: "Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizi. Na fanyeni wema. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema." [Qur'an, 2:195].

Kuna njia kuu za kiasili za kujipatia mali, kama vile kuajiriwa au kuajiri, biashara, ufugaji, kilimo, viwanda au ufundi. Njia hizi zote ziko katika hukumu ya uhalali, kwa mujibu wa Jopo la Wanazuoni wa Sharia ya Kiislamu. Kadhalika zipo njia za halali zisizo za kudumu au za kawaida za kujipatia mali. Baadhi yake hupatikana bila malipo au mbadala, kama vile mirathi, zawadi, sadaka, mahari, n.k.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

شَعْبَان

SEHEMU YA 3



# SIMULIZI ZA AKINA ADI, WATU WA HUD

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Katika Makala iliyopita tuliona namna kina Adi walivyopinga mafunzo ya Mtume wao, Hud. Walimkejeli wakimwambia: "Ewe Hud, sisi tumekuwa tukikusikia mara nyingi ukitaja adhabu, iko wapi na lini itafika?!" Kisha wanamcheka vicheko vya kukohoa – kwa kiburi kikubwa na kujiamini - wakawa wanasubiri adhabu kama alivyowaahidi Hud iwapo watakaidi maagizo ya Mola wao.**

### Mtume Hud ashangazwa na kauli zao

Mtume Hud (Allah amshushie rehema na amani) aliwashangaa sana watu wake kwa kujitia ujasiri na kudhani kwamba hakuna atakayewaadhibu.

Hud aliwasikitikia sana na hakuzidisha zaidi ya neno lake: " Innamal 'ilmu 'indallaahi wa innamaaa ana naziirum mubiin " (Hakika elimu yote iko kwa Allah na mimi si zaidi ya kuwa muonyaji mbainishaji).

Adhabu ya Allah kuwashukia kina Adi

Adhabu ya Allah kwa Adi ilianza kwa kukoseshwa mvua kwa kipindi kirefu na joto kali lililoenea nchi nzima, hadi wakawa na haja na shauku kubwa ya kupata mvua.

Basi kuna siku moja wakaona wingu limetanda juu, na kwa kuwa walikosa mvua kwa muda mrefu, walifurahi sana. Basi wakawa wanapigiana kelele za matumaini na kuitana wakisema, "Wingu hili hapa litaleta mvua." Watu wakacheza na kufurahi.

Lakini Mtume Hud alijua kwamba, wingu lile halikuwa la mvua na rehema, bali lilikuwa la adhabu. Alijua Allah anataka kuwaadhibu wababe hao na – kwa kweli- ilikuwa ni siku yao ya kuwaonesha kwamba kuna nguvu kubwa inayowatawala na kuutawala ulimwengu wote, imekasirishwa na maovu yao, na nguvu yenyewe ni Allah Ta'ala.

Lilikuwa ni wingu la upepo mkali wa ajabu. Qur'an inasema: "Basi, walipoliona wingu likiyaelekea mabonde yao walisema, 'Wingu hili la kutunyeshea mvua' (wakaambiwa) 'Bali haya ni yale mliyokuwa mkiyaharakisha, ni upepo ambao ndani yake mna adhabu iumizayo.' Utaangamiza kila kitu kwa amri ya mola wake..." [Qur'an, 46: 24-25].

### Adhabu ilivyokuwa

Wakati wa kuadhibiwa ulipofika, ulivuma upepo wa kimbunga wa ajabu haujawahi kutokea na kuonekana katika historia ya mwanadamu.

Upepo ule ulin'goa miti mirefu, ukavunja majumba na makasri yao. Uliwainua wanyama juu masafa marefu, kisha kuwatupa mbali kabisa wakiwa vipandevipande!

Michanga na changarawe za majangwani zikaruka kwa kasi, dunia ikakumbwa na giza la upepo wa adhabu na mawingu. Watu wakakimbilia majumbani mwao na kujifungia milango; watoto wakawakumbatia mama zao, watu wazima wakazikumbatia kuta za vyumba vyao.

Vilio vya watoto wakilia na wanawake wakipiga makelele ya kuomba msaada vilisikika – na hakika hofu ilitawala katika maeneo yote!

Qur'an inasimulia: "Basi Adi walitakabari katika ardhi bila ya haki na wakasema, 'Nani aliye na nguvu zaidi kuliko sisi? Je hawakuona ya kwamba Mwenyezi Mungu aliyewaumba ndiye Mwenye Nguvu zaidi kuliko wao, wakawa wanazikanusha aya zetu."

"Basi tukawapelekea kimbunga katika siku za shari (kwao) ili tuwaonjeshe adhabu ya khizaa (fedheha) katika maisha ya dunia, na adhabu ya akhera ni ya kufedhehesha zaidi, nao hawatonusuriwa." [Qur'an, 41:15-16].

Katika pahala pengine Qur'an inasimulia: "Na ama Adi waliangamizwa kwa upepo mkali usiozuilika. Aliowapelekea misiku saba na michana minane moja kwa moja bila ya kusita. Utawaona watu wameanguka (kifudi fudi) kama magogo ya mitende matupu. Basi je unamuona mmoja wao aliyebaki?!" [Qur'an, 69:6-8]

Basi hivi ndivyo walivyoangamizwa watu wa Mtume Hud na kubaki tu historia na kumbukumbu zao katika maandiko. Na inaposemwa: "Basi je unamuona hata mmoja tu aliyebakia!?", inamaanishwa kwamba, watu hao madhalimu adhabu iliwasaga na kuwamaliza wote isipokuwa wachache waliomuamini na kumtii Mtume wao.

Qur'an [11:58-60] inasema: "Ilipofika amri yetu (ya kuangamizwa), tulimuokoa Hud na wale walioamini pamoja naye kwa rehema itokayo kwetu na tukawaokoa katika adhabu ngumu. Na hao ndio Adi. Walikanusha aya za Mola wao na wakawaasi Mitume yake, na wakafuata amri ya kila jabari mkaidi. Na wakafuatishiwa laana katika dunia hii na siku ya kiyama. Sikilizeni, hakika Adi walimkufuru Mola wao, sikilizeni, wakaangamizwa, hao Adi watu wa Hud."

Kuangamizwa kwa akina Adi kunatoa funzo kubwa kwamba, mwisho wa madhalimu wanaoendelea kukaidi maagizo ya Allah ni mbaya na adhabu haitoishia hapa duniani tu.

Kisa kinatuonesha kuwa, wanadamu wa leo ni dhaifu sana kuliko hao wa zamani.

Allah A'alam.

شَعْبَان

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Namna bora ya kumwandaa mtoto kuikabili Ramadhan



**Kati ya mambo ambayo wazazi na walezi wengi wa Kiislamu hukosea ni kutowazoesha watoto kufunga swaumu ya wajibu ya Ramadhan na zile za Sunna wangali wadogo. Hali hii ndiyo inayopelekea baadhi yao kushindwa kufunga hata wanapokuwa wakubwa.**

Tofauti na wazazi wengi wa sasa, Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani iwe juu yake), kwa watoto alikuwa ni baba mwenye upendo na huruma, mlezi mwenye busara, akiwazoesha kufanya ibada mbalimbali ikiwamo funga na sala. Alifanya hivyo akijua kuwa utoto ni kipindi nyeti na muhimu kwa mzazi/mlezi kupandikiza kwa mtoto wake misingi ya imani, maadili, tabia njema, heshima na nidhamu.

Mtume ameelekeza wazazi na walezi kuwafundisha watoto wao matendo ya ibada wakifikisha umri wa miaka saba, aliposema: "Waamrisheni watoto wenu kusali wakifikisha miaka saba, na wapigeni wakifiksha miaka 10 (kwa kutosali), na muwatenganishe kwenye vitanda." [Sunan Abi Daudi].

Aidha, ukidadisi malezi ya Masahaba (Allah awaridhie wote) kwa watoto wao, utaona walikuwa wakiwapa mazoezi ya kufunga wangali bado wadogo. Wanazuoni wengi wana maoni kwamba umri ambao mtoto anapaswa kuanza kufunga ni kati ya miaka 10 na 12.

Hata hivyo, tahadhari inapaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa hakuna madhara kwa mtoto wa umri huo kufunga. Kwa watoto ambao hawajawahi kabisa kufunga, kwa kawaida wengi wao huanza hatua kwa hatua ili kuhakikisha wanazoea kukaa na njaa na kiu kwa muda mrefu.

### Kauli za wanazuoni kuhusu suala hili:

Mwanazuoni Al–Awzaaiy (Allah amrehemu) amesema: "(Mtoto) akiweza kufunga siku tatu mfululizo bila ya kukatiza na bila ya kudhoofika, basi alazimishwe kufunga Ramadhan."

Mwanazuoni mwingine aitwae Is–haq amesema: "(Mtoto) anapofikisha umri wa miaka 12 nadhani alazimishwe kufunga ili azowee. Umri wa miaka 10 inawezekana zaidi, kwa sababu Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake) amefaradhisha adhabu nyepesi kwa watoto wanaoacha sala katika umri huu. Na kwa vile kufunga pia ni nguzo muhimu ya Uislamu, kwa umri huo inaonekana anaweza kufunga..." [Taz: 'Al–Mughni,' juz. 4, uk. 412].

Kwa upande wake, Sheikh Ibn Uthaymiyn (Allah amrehemu) amesema: "Iwapo (mtoto) ni mdogo na bado hajabalehe haimlazimu kufunga, lakini ikiwa ana uwezo wa kufunga bila ya taabu (wala kudhurika), basi aambiwe afanye hivyo, kwani Masahaba (Allah awaridhie) walikuwa wakiwafungisha watoto wao, na wale wadogo walipokuwa wanalia waliwapa wanasesere ili kuwashughulisha." [Taz: 'Majmuu' Fataawal–Shaykh Ibn Uthaymiyn,' juz. 19, uk. 83].

Jambo muhimu la kuzingatia katika masuala haya ni kwamba, swaumu ya mtoto ni mustahab (imependekezwa) na si wajibu. Mtoto akifunga analipwa thawabu na akiacha kufunga hapati madhambi. Hata hivyo inatakikana kwa mzazi au mlezi kumuamrisha kufunga ili azowee. Miongoni mwa mbinu za kumzoesha mtoto kufunga ni kuifanya funga iendane na utoto wake. Ukitaka kumzoesha kufunga kwa ukali na kutaka aache michezo aliyoizoea ataichukia funga na hutafikia lengo. Wapo watoto wanaoanza kufunga kwa saa kadhaa mpaka hufikia kumudu kufunga siku nzima.

Kisha huanza kufunga baadhi ya siku za Ramadhan, na kuacha nyingine, hivyo hivyo mpaka wanamudu kufunga. Hali kadhalika, wapo watoto wanaoanza kufunga huku wakidokoa vitu vidogo vidogo au kunywa maji kwa kificho. Hawa wataacha tabia hii taratibu kadri wanavyozoea kufunga na kukua.

Ili kuwavutia watoto kufunga ni vizuri kuwaandalia futari wanayoipenda, kadri Allah alivyokujaalia na kuwapa zawadi kwa kila hatua wanayopiga kuelekea kuimudu funga.




MAKALA MAALUM

0773 181 494

MUSSA IMANI SHEHA, ZANZIBAR

# Ujumbe kwa Wasomi Waislam

**Uislamu ni dini ya elimu, na imepiga vita ujinga tokea mwanzo wa risala (ujumbe) yake kwa walimwengu. Aidha, Uislamu umehimiza kusoma elimu zote zenye manufaa kwa mwanadamu.**

**Uislamu hautenganishi elimudini na elimudunia. Kila elimu ina nafasi yake katika maisha ya mwanadamu alimradi iwe kwa ajili ya Muumba. Na mtaalamu wa fani yoyote ni hitajio la jamii inayomzunguka kwa ustawi wake.**

**Lakini kuna elimu ya msingi na ambayo kila Muislamu anapaswa kuijua, nayo ni elimu ya dini, ambayo ndio muhimili na msingi wa elimu zote.**

**Hii ni elimu ya kumtambua Allah Muumba na ulazima wa kumtumikia. Elimu ya kumjuvya mwanadamu haki na majukumu yake kwa viumbe wenzake kiimani, na kumuongoza kuwa na tabia njema, na kujali shida za wengine.**

## Hali ya jamii

Jamii leo inaonekana kuvutika sana na elimu ya mazingira ama "elimuajira." Juhudi wanazozifanya wazazi za kuhakikisha watoto wao wanaipata elimu ya mazingira hatimae kupata ajira ni kubwa sana, na huanza mapema kabisa. Hupitia ngazi zote: maandalizi, msingi, sekondari hadi chuo.

Lakini kwa upande wa masomo ya dini, juhudi hizi hazionekani sana - si kwa wazazi wala kwa hao watoto na vijana wenyewe waliokwisha kuisoma picha na kujua nini haswa wanachokihitajia wazazi wao.

## Matokeo yake

Matokeo ya upuuzaji huu mkubwa wa elimu ya kiroho ni kuwa na idadi kubwa ya wasomi Waislamu, bobezi katika fani mbali mbali katika elimu ya mazingira lakini wana uelewa mdogo sana kuhusu dini yao.

Aghlab, mambo huharibika na haki za watu kupotea pale wasomi hao wanapopewa dhamana ya kuwa viongozi na watumishi wa umma kama wanasiasa, madaktari, walimu, viongozi wa umma, askari, walinzi, wanahabari, mahakimu, wanasheria, mawakili nk.

Utashi na tamaa za kujipatia maslahi, huushinda utu, huruma na kujali shida za watu. Uzembe, utapeli, rushwa, majungu na hata ushirikina kazini, uongo, na hiyana: huwatawala wasomi hao.

Pia, hawasalimiki na wizi wa mali ya umma pale wanapoamini kuwa hakuna jicho la mtu au chombo cha sheria kinachowamulika . Jamii yenye wasomi na watendaji kama hao hujikuta inanyonywa na kubeba mzigo mzito usio na faida kwake, na maisha ya wanajamii kuwa magumu zaidi.

Upuuzaji wa maagizo ya Allah –kama vile swala- kwa wasomi hao ni kitu cha kawaida. Baadhi yao hufikia hatua ya kuwadharau waliosoma dini, wakajawa na kibri na kutoa lugha za kejeli dhidi ya Uislamu (dini yao wenyewe) na viongozi wake.

Wasomi hao hujiliwaza: eti kwa vile wamesoma sana fani zao mbali mbali, basi hata dini nayo wanaijua, na wana uwezo wa kuisemea wakitaka wakitegemea mantiki badala ya Qur'an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

## Kuathirika na umagharibi

Mtihani zaidi ni wasomi hao kuathiriwa na nadharia za wasio Waislamu (hasa ulimwengu wa kimagharibi) wakawapenda na kuwasifia kuliko Waislamu wenzao.

Huzimeza historia, tafiti na nukuu za watafiti na vumbuzi zao, lakini wanashindwa kujua historia ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) na Maswahaba wake (Allah awaridhie), wala hawawezi kunukuu aya, hadith au kauli za wataalamu (wasomi) wa Kiislamu.

Tazama ndugu zetu hawa –Allah atuongoze sisi na wao-wanavyokuwa wageni siku zote katika utekelezaji wa ibada misikitini. Naam, kwa sababu hawajifunzi na wala hawana mpango wa kujifunza!

Pitia darsa za misikitini, mihadhara ya dini pamoja na taasisi za maarifa ya Uislamu, halafu angalia washiriki wa programu hizo ni akina nani? Hatutarajii kwamba, utawaona wengi katika waitwao wasomi na ambao wana ajira (nyadhifa) zao kubwa kubwa au wenye vipato vikubwa (matajiri).

Haitarajiwi pale kuwakuta: wakurugenzi, makatibu wakuu, wabunge, mawaziri, maafisa, mameneja, wakuu wa mikoa na wilaya nk. ambao ni waislamu, ambao walipaswa pia kujifunza na kuijua vyema dini yao!!

## Wito

Tunatoa wito kwa wazazi kuwapeleka watoto wao katika taasisi za elimu ya dini (madrasa na ma'had) wakajifunze imani iwasaidie katika kujenga mahusiano mema na Mola wao, na kuwa raia wema wasiwe mzigo kwa wanajamii wenzao.

Tunawaambia ndugu zetu waliosoma elimu ya mazingira (sekula) na kushika nyadhifa mbali mbali, na ambao hawakubahatika kuijua dini yao: bado hawajachelewa.

Muda bado upo na wajibu uko pale pale. Wajishuhulishe na kuisoma dini yao kwa namna majukumu yatakavyowaruhusu. Kuweni karibu na wasomi wa dini mubadilishane uelewa kwani elimu ni bahari.

Saidianeni katika kuwaongoza watu njia iliyo sahihi. Jamii inawategemea sana, ioneeni huruma. "Mbora wa watu ni awatumikiae watu."

شَعْبان

AFYA YAKO

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Wafanyakazi wengi hatupati mapumziko ya kweli ya akili



Katika maeneo mengi ya kazi, kupumzika ni neno rahisi kusema lakini gumu kutekeleza. Wafanyakazi wengi wamelelewa kwenye utamaduni unaosifu "kujituma bila kikomo": saa ndefu, majukumu mengi, na kuishi kana kwamba uchovu ni ushahidi wa uaminifu na ubora. Ukweli ni huu: kazi bora haiwezi kudumu kutoka kwa akili na miili iliyochoka.

## Kupumzika si usingizi tu

Watu wengi huamini kupumzika ni kulala tu ndiyo maana mtu anaweza kupata usingizi wa kutosha lakini bado akajisikia amechoka na mzito kiakili. Usingizi hupumzisha mwili, lakini mapumziko ya kweli yanahitaji pia akili na hisia zipate nafasi ya kushusha kasi.

Unaweza kuwa kitandani, lakini mawazo yakaendelea: yakipanga majukumu ya kesho, yakirudia makosa ya leo, au yakihangaikia mitazamo ya watu. Kupumzika halisi ni zaidi ya kulala; ni kuhama kutoka "kufanya" kwenda "kuwa," na kuiacha akili ipumue bila kusukumwa na taarifa, kelele na presha.

## Tunafungwa na simulizi za ndani

Sababu kubwa inayofanya mapumziko yawe magumu ni pale mtu anapounganisha thamani yake na alichokamilisha. "Nikifanya mengi, mimi ni wa maana zaidi." Hapo mapumziko huonekana kama tishio kwa utambulisho: ukipumzika, unaonekana umepungua thamani, umekuwa mvivu, au umepoteza nafasi ya kusonga mbele.

Kuna pia hofu ya mitazamo ya watu: "Wataniona mzembe," "nitaonekana siwajibiki," au "nitawakwaza wenzangu." Hata akiwa amechoka, mtu huendelea na kazi kwa hofu ya lawama au kupoteza sifa njema. Matokeo yake ni kufanya kazi kwa kujilazimisha, si kwa utulivu wa ndani.

## Kupumzika kunapotupeleka kukutana na nafsi zetu

Kwa wengine, tatizo si muda wa kupumzika, bali ni hisia zinazojitokeza mtu anapopumzika. Ukikaa kimya, unaweza kukutana na upweke, huzuni, wasiwasi, hasira, au maswali ya maisha yaliyokuwa yakizimwa kwa "busy."

Hapo kazi inageuka kimbilio, na mapumziko yanaonekana hatari kwa sababu yanakutoa kwenye mwendo unaokufanya usizifikirie changamoto zako. Hii ni moja ya sababu wengi huahirisha kupumzika. "Nitapumzika baadaye" mara nyingi huishia kuwa "sitapumzika."

## Mapumziko bandia

Changamoto nyingine ni kuchanganya mapumziko na kuzimia kiakili. Baada ya kazi, mtu anaweza kukaa na simu, akiteleza mitandaoni au kutazama video mfululizo.

Kwa nje anaonekana amepumzika, lakini akili bado inamezwa na msisimko wa taarifa na ulinganisho wa maisha. Hali hii inaweza kuongeza uchovu, kwa kuwa ubongo unaendelea kuchakata, kuhukumu na kuvutwa huku na huko.

Kupumzika halisi si lazima ikugharimu bali vitu rahisi kama vile kukaa bila skrini, kutembea taratibu, kutazama machweo, kusoma kwa utulivu, kuandika mawazo, kuzungumza na familia kwa umakini, au kutumia muda wa ibada kwa utulivu unaokusanya nafsi. Haya ndiyo mapumziko yanayorudisha nguvu ya ndani, si kubadilisha tu aina ya kelele.

Teknolojia imefanya kazi kuwa "ya saa 24"

Katika maisha ya sasa, kazi imeingia mfukoni. Barua pepe, vikundi vya kazi, simu za haraka na ujumbe wa "tafadhali cheki hili" huja hata baada ya muda wa kazi. Hapo akili hukosa mpaka wa kusema, "Sasa nimeondoka kazini." Ukikosa mpaka huo, hata ukiwa nyumbani, bado upo kazini kiakili.

Kupumzika kunahitaji kujitenga. Hii si uvivu; ni kuweka mipaka inayolinda afya ya akili na ufanisi wa muda mrefu: kuwa na saa maalumu za kuangalia ujumbe wa kazi, kuweka muda wa ukimya wa simu, au kutenga dakika chache za kupumua kabla ya kuingia majukumu ya nyumbani.

## Kupumzika ni msingi wa tija, si adui yake

Wapo huamini kupumzika kunapunguza uzalishaji lakini ukweli ni kinyume chake: akili ikipata nafuu, umakini huongezeka, ubunifu hurudi, maamuzi huwa bora, na makosa hupungua.

Mabadiliko huanzia kwenye kujikumbusha kwamba kupumzika si kitu cha "kupewa" na kazi, bali ni haki ya mwili na nafsi.

Kadri unavyojifunza kupumzika, ndivyo unavyogundua ukweli muhimu, kwamba, kupumzika si mwisho wa safari ya kazi; ni sehemu ya njia ya kuifanya kazi iwe endelevu, yenye baraka na yenye afya.

NA ZAHARANI BARAKA




# Sikumjua aliye mbali na msikiti zaidi yake

**Imepokewa hadith kutoka kwa Ubayy bin Ka'b (Allah amridhie) akisema: "Alikuwepo mtu mmoja katika Answar, na sikumjua yeyote aliye mbali zaidi na msikiti kuliko yeye. (Mtu huyo) hakukosa sala (ya jamaa) hata moja, akashauriwa anunue punda wa kumpanda wakati wa giza (la usiku) na wakati wa joto kali. Mtu yule akasema: "Sifurahishwi nyumba yangu iwe karibu na msikiti. Mimi nataka niandikiwe (thawabu) za hatua zangu za kwenda msikitini na ninaporejea kwa watu wa nyumbani kwangu." Mtume (rehema na amani zimshukie) akasema: "Hakika Allah amekukusanyia hayo yote." *[Imepokewa na Muslim]***

## Mafundisho ya tukio hili

Kuimarisha nafsi katika utiifu na kudumisha kutekeleza mambo ya wajibu katika mazingira yoyote yale ni miongoni mwa matendo bora zaidi kwa Muislamu. Nafsi ya mwanadamu huchoka na kuzembea katika kumtii Allah hivyo huhitaji utakasifu unaosababishwa na mapambano ya mja baina yake na nafsi yake katika kuiteza nguvu na kuilekeza katika twaa.

Imani ya mja haikamiliki sawasawa ila kwa subira na kuizuia nafsi isiteleze katika mambo ya haramu, na kuwa na bidii katika yale ambayo nafsi inayaona kuwa ni mazito. Wenye hekima wamesema: "Nafsi ni kama mtoto, usipomzuia (kunyonya), atakua huku akiwa anapenda kunyonya; na ukimnyima (ukaacha kumnyonyesha) ataacha."

Mja anapovumilia, akadumu katika utekelezaji wa maamrisho ya Allah kwa namna yake sahihi, akaizuia nafsi yake kufanya maovu huku akipambana na yale magumu yanayoweza kuitia uzito nafsi, hujiona mtulivu na mwenye faraja moyoni, na huona mambo mazito kuwa ni mepesi.

Mja wa aina hii huyachukia maasi, hatimaye huonja ladha ya ibada na kuyaona mepesi mambo ambayo watu wengine wanaona kuwa ni magumu. Mwenyezi Mungu anasema: "Lakini Allah amekupendezesheeni imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na akakuchukizeni ukafiri, ufasiki na uasi. Hao ndiyo walioongoka sawasawa." [Qur'an, 49:7].

Mhusika wa tukio hili anawakilisha kizazi kitukufu kilichoimarishwa na mafunzo ya Uislamu. Unaloliona zito kwako katika kuufanyia kazi Uislamu, kwao lilikuwa jepesi mno. Umma wetu hivi sasa unahitaji watu wanaotambua kuwa wao ni matofali madhubuti katika kuimarisha jengo la umma.

Hii ni kwa sababu, kuharibika kwa umma kunatokana na kuharibika kwa watu wake; na kutengamaa au kuimarika kwa umma ni kule kuimarika kwa watu wake. Allah Mtukufu amekisifia kizazi bora kilichowahi kuishi katika umma huu ndani ya karne zinazosifika kwa kila aina ya ubora, kizazi kilichojua kwa uhakika wake maana ya tamko la 'Lailaha illaLlah; Muhammadu rrasuluLlah'.

Wao walifanyia kazi yale yote yaliyomo kwenye tamko hili na siyo kulitamka tu kwenye ndimi zao. Tamko hili halikuwa jepesi na la mpito kwao kama ilivyo kwa Waislamu wengi wa sasa, ambao hulitamka kwa wingi huku uhalisia wa maisha yao ukiwa kinyume kabisa na matakwa ya tamko hili.

Ndiyo maana Allah amekisifia kizazi hiki bora kilichoishi katika karne bora kwa kusema: "Nyinyi mmekuwa umma bora kabisa uliotolewa (mfano) kwa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu..." [Qur'an, 3:110].

Hii ni kwa sababu, wao walilitambua neno hili na wakalipa haki yake inayostahiki, waliunda jamii ya kiimani yenye haiba yenye nguvu, hatimaye ukapatikana umma uliosimama katika misingi ya imani moja ya kumtakasia ibada Allah peke yake na kumfuata Mtume ipasavyo.

Jamii hii ilitosheka na kumfanya Mtume (rehma za Allah na amani zimshukie) kuwa ndiye kigezo chao na kiongozi wao katika kila kitu, jambo ambalo liliwafanya wapandishwe daraja kubwa ya kupewa uongozi na mamlaka katika ardhi. Hiyo ndiyo ahadi ya Allah kwa wale watakaopita njia ya sawasawa katika imani na kutenda yaliyo mema.

"Allah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya Makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya Makhalifa waliokuwa kabla yao. Na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya hofu yao, wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndiyo wapotovu." [Qur' an, 24:55].

Hivyo, kinachotakiwa ni kuziimarisha nafsi zetu ili tuwe na umma mmoja uliojengeka katika misingi ileile ya mwanzo, jambo litakalotupandisha daraja na kurejea katika nafasi yetu ya kuwa umma bora. Sahaba tunayemzungumzia katika tukio hili hakuwahi kukosa sala ya jamaa, lakini Muislamu wa leo anaweza akakosa kusali jamaa msikitini ilihali msikiti upo jirani kabisa na nyumba yake.

## Pande mbili za nafsi

Tukitazama mafundisho ya Uislamu, tunakuta nafsi ina pande kuu mbili. Upande wa kwanza ni ule wa maumbile ya asili, uliosalimika, na wenye kumtambua Allah, umeumbwa katika kupenda haki na kheri, na umewekewa maandalizi ya kuitambua haki na kuifurahia, na inasikitika pale inapokwenda kinyume na haki.

Lau kama si kuwapo kwa mvutano na upinzani, basi nafsi ingebakia katika asili yake, watu wote wangesimama katika mstari ulionyooka kimatendo na kitabia. Haya ni maarifa ya kimaumbile ambayo Allah ameyaweka kwenye nafsi na yanamsaidia mtu kuitofautisha haki na batili.

Upande wa pili wa nafsi unapingana na upande mzuri wa kimaumbile, ambao hudhoofisha na kuugeuza katika mila za kufru na shirk kutokana na ushawishi, udanganyifu na mambo mbalimbali, yakiwamo mazingira anayokulia mwanadamu tangu akiwa mtoto.

Katika hadithil Qudsy, Allah Mtukufu anasema: "Hakika mimi nimewaumba waja wangu wote wakiwa katika mila iliyo sawa, na hakika wao shetani aliwajia akawapondosha katika dini yao na akawaharamishia waliyohalalishiwa na akawaamrisha wanishirikishe kwa yale ambayo sijayateremshia ushahidi." [Muslim].

IDARA YA DAAWA

# Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

شَعْبَان

MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Mbinu za malezi chanya kwa mama wa Kiislamu

Malezi chanya ni safari ya kujenga uhusiano wa karibu na wa kudumu kati ya mzazi na mtoto kwa misingi ya heshima, mawasiliano na mfano mwema.

Katika Uislamu, mtoto si mali ya mzazi bali ni amanah kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka. Hivyo, jukumu la mzazi—hasa mama ambaye mara nyingi huwa karibu zaidi na mtoto—ni kumlea mtoto kwa upendo, busara na mwongozo unaomwandaa kuwa binadamu bora duniani na Akhera.

Malezi chanya yanasisitiza kumlea mtoto kwa msukumo na uthibitisho chanya badala ya hofu na ukali. Mtoto anapaswa kuheshimiwa kama mtu binafsi mwenye hisia, fikra na utu wake. Badala ya mtazamo wa "fanya kwa sababu nimesema," Uislamu unahimiza maelezo, majadiliano na kueleweshana kulingana na umri wa mtoto.

Ingawa malezi hubadilika kulingana na hatua za ukuaji wa mtoto, misingi yake inaweza kutumika katika umri wowote.

## Ukweli katika hali zote

Kwanza kabisa, ukweli ni nguzo muhimu ya malezi chanya. Watoto hujifunza zaidi kwa kuangalia wazazi wao kuliko kusikiliza wanachosema. Mama anaposema uongo, hata kwa mzaha au kwa lengo la kumtisha mtoto, humfundisha mtoto kuwa uongo ni njia halali ya kutatua mambo.

Ahadi hewa, vitisho vya kubuni na kauli zisizotekelezwa huvunja imani. Hata pale ambapo ukweli unapokuwa hauwafai watoto kwa umri wao, ni busara kuwaambia kwa uaminifu kuwa watapewa maelezo wanapokuwa wakubwa.

## Mapenzi ya dini

Ni muhimu pia kumtambulisha mtoto katika Uislamu kwa njia ya kupendeza itakayomfanya aupede Uislamu. Dini isiwasilishwe kama mzigo au adhabu, bali kama chanzo cha faraja na furaha.

Kusikiliza Qur'an, kujifunza dua fupi, kusimuliwa hadithi za Manabii na kuzoea taratibu za Kiislamu mapema hujenga uhusiano wa mapenzi na imani. Mtoto anayefurahia kujifunza dini hukua akiipenda bila kulazimishwa.



## Mazungumzo

Mazungumzo ni mhimili mwingine wa malezi chanya. Mtoto anapaswa kuzungumziwa kwa heshima, kwa sauti ya upole na kwa lugha anayoielewa.

Kukaa chini na kuzungumza naye uso kwa uso huonyesha huruma na kuthamini mawazo yake. Mazungumzo ya kila siku kuhusu maisha, mipango na hisia huwasaidia watoto kujifunza kwa urahisi na kujenga ujasiri wa kuwasiliana.

## Usalama wa kihisia

Nyumbani panapaswa kuwa mahali pa utulivu na usalama wa kihisia. Kelele, matusi na migogoro ya wazazi mbele ya watoto huathiri sana afya ya kisaikolojia ya mtoto. Mtoto anayekulia katika mazingira ya amani hujenga utulivu wa ndani. Pale mzazi anapochoka au kukerwa, ni busara kuchukua muda wa kupumzika kabla ya kushughulikia mtoto.

Malezi chanya pia yanahusisha kuangazia mema kuliko mabaya. Mtoto anapofanya jambo jema, pongezi humjenga zaidi kuliko lawama za mara kwa mara. Badala ya kuwatisha watoto kwa adhabu, ni bora kuwaeleza faida za kufanya jambo sahihi. Mtazamo huu huwasaidia kujenga motisha ya ndani.

## Stadi za maisha

Kadhalika, watoto wanapaswa kuzoeshwa katika mtindo wa maisha wa wazazi badala ya wazazi kubadilisha maisha yao yote kwa ajili ya watoto. Kwa kutafuta suluhisho za kuwajumuisha watoto katika shughuli za wazazi, watoto hujifunza kubadilika na kushiriki.

Hii huenda sambamba na kuanzisha tabia njema mapema kama kusoma, kula vyakula vyenye afya, kusalimia watu na kupenda hadithi.

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS




# Paranoia: ni zaidi ya hofu ya kawaida

Katika mazungumzo ya kila siku, watu wengi hutumia neno "paranoia" kumaanisha kuogopa, kuwaza mabaya, au kuwa na wasiwasi mwingi. Hata hivyo, kwa upande wa afya ya akili, paranoia si sawa na hofu ya kawaida wala si sawa na wasiwasi wa aina ya "ninaogopa mambo yataenda vibaya."

Paranoia ni dhana ya kisaikolojia inayohusisha kiwango cha juu cha tuhuma, tafsiri potofu za nia za wengine, au imani nzito kwamba kuna tishio linalokulenga moja kwa moja, hata pale ushahidi wa wazi haupo.

Ili kuielewa vizuri, paranoia fikiria tofauti hii: Wasiwasi wa kawaida huleta wazo la "itakuwaje kama..." na mtu anahofia jambo baya litatokea. Paranoia, kwa upande mwingine, huleta hisia na tafsiri ya "kuna mtu au kitu kinaniwinda," au "wanafanya jambo fulani kwa makusudi dhidi yangu." Hali hii huanza polepole na kisha kuota mizizi.

Kuna partanoia hutokewa kwa muda mfupi, hali ambazo karibu kila mtu anaweza kuipata kwa sababu zinazoeleweka. Fikiria mtu aliyelala peke yake kwenye kambi ya mbali, usiku ukiwa kimya, watu wachache sana, kisha wageni wawili wanafika na kuanza kuuliza maswali, ikiwemo kama yuko peke yake.

Baadaye usiku, mmoja wao anatoka nje na kuzunguka huku na huko, na mazingira yanazidi kuonekana ya ajabu. Mtu huyo anaweza kuingiwa na tahadhari kali, kushindwa kulala, na hatimaye kuamua kuondoka haraka.

Katika mazingira hayo, tahadhari hiyo ni ya kujilinda; ni mwitikio unaoweza kuwa wa busara kwa sababu kuna viashiria vinavyoweza kuonyesha hatari. Lakini vipi kuhusu mtu ambaye kila siku anajihisi hivyo, hata akiwa nyumbani, kazini, au kwenye mazingira salama? Hapo paranoia huwa imevuka mipaka ya "tahadhari ya kawaida" na kuwa tatizo linalohitaji uelewa na msaada.

Paranoia inaweza kuhusiana na historia ya kiwewe, namna mtu alivyojengeka kitabia, au hali za kisaikolojia zinazoambatana na upotovu wa mtazamo wa uhalisia.

Kadiri siku zinavyopita, mawazo ya tuhuma "huingia kwenye maisha" na kuanza kuchorea picha ya jumla: mtu anaona hatari, hila au uadui katika maeneo mengi zaidi ya maisha yake. Hatimaye, paranoia inaweza kujionesha kwa sura tatu kuu.

## Paranoia ya kiwewe (trauma)

Sura ya kwanza ya paranoia ile inayotokana na kiwewe na msongo baada ya tukio la kutisha, ambapo mtu anaweza kuishi katika hali ya "hypervigilance," yaani kuwa macho kupita kiasi kwa mazingira, tayari kupambana au kukimbia.

Kwa waliopitia mazingira ya hatari ya muda mrefu, akili hujifunza kwamba kuwa makini ni lazima ili kuishi. Hata sauti ndogo, kivuli, au mlio wa upepo unaweza kumfanya mtu aingiwe na wasiwasi mkubwa na kutafsiri ishara ndogo kama tishio.

Hapa, hofu ya asili ya kujilinda inaweza kukomaa hadi kuwa na ladha ya paranoia, kwa sababu mfumo wa ulinzi wa ubongo unakuwa mkali kupita kiasi na hushindwa "kuzima" hata baada ya hatari kuisha. Mbinu za kutuliza mwili na akili, kama mazoezi ya kujiweka kwenye sasa, utulivu wa kupumua, na uangalifu wa makusudi (mindfulness), mara nyingi husaidia kupunguza makali ya hali hii.

## Paranoia ya tabia/muundo wa utu

Paranoia ya pili ni ile inayotokana na muundo wa utu, yaani tabia ya kutoamini na kutia shaka kupita kiasi. Katika hali hii, wasiwasi ni mtindo wa maisha. Mtu huamini mtu wa karibu anataka kumtumia, sifa nzuri hutafsiriwa kama hila ya kutaka faida, na maoni ya kawaida huonekana kama kejeli au dharau.

Mtu anaweza kujenga ukuta wa umbali na ubaridi ili kuzuia watu wasimkaribie aghlabu kutokana na historia ya kuumizwa mapema maishani, na hivyo kujifunza kutokuamini ili wasiumizwe tena.

Changamoto kubwa ni kwamba, kwa sababu ya kutokuamini kwao, si rahisi wao kuingia kwenye tiba; badala yake, huenda wale walioko karibu nao ndio wanaohitaji msaada wa namna ya kuishi nao bila kuumizwa.

## Paranoia ya kidanganyifu

Hii inatokana na magonjwa ya kisaikolojia yanayopeklekea kupoteza mwelekeo wa uhalisia, kama sonona. Hapa, mtu anaweza kuwa na imani isiyoyumba, isiyo sahihi, na isiyorekebishika kwa maelezo ya kawaida.

Imani hizi mara nyingi hujengwa kwenye



# Safari ya wazo la bidhaa hadi sokoni: Hatua 6 muhimu

**Wazo la biashara linaweza kuwa dogo mwanzoni, lakini likiandaliwa vizuri linaweza kugeuka kuwa bidhaa inayohitajika sokoni. Wajasiriamali wengi hushindwa si kwa kukosa mawazo, bali kwa kukosa mwelekeo na mpangilio wa hatua za kufuata. Ili wazo liwe bidhaa halisi, inayokubalika na wateja, ni lazima kupitia mchakato unaohitaji fikra pana, majaribio, na utayari wa kujifunza. Makala inataja hatua hizo muhimu.**




## Kwanza: Weka dira iliyo wazi

Hatua ya mwanzo ni kutengeneza dira ya bidhaa yako itakayotaja nani unayemlenga, tatizo gani bidhaa yako inatatua, na kwa nini mteja achague bidhaa yako badala ya nyingine zilizopo sokoni.

Maswali haya huweka msingi wa maamuzi yote ya baadaye, kuanzia bei hadi ujumbe wa matangazo.

Ni muhimu pia kutafiti soko mapema. Wateja huonyesha mahitaji yao kupitia tabia zao za manunuzi, maoni, na majadiliano ya mitandaoni. Kukusanya taarifa mapema hukusaidia kurekebisha wazo kabla hujatumia rasilimali nyingi.

## Pili: Tengeneza toleo la awali la bidhaa

Baada ya kuwa na dira, hatua inayofuata ni kutengeneza toleo la awali la bidhaa. Hili ni jaribio la kwanza la bidhaa lenye sifa muhimu tu, linalolenga kujaribiwa na watumiaji halisi. Lengo hapa si ukamilifu, bali kujifunza haraka.

Majaribio ya bidhaa hukusaidia kugundua changamoto za matumizi, ubora, au muundo. Mara nyingi bidhaa huonekana nzuri kwenye mipango, lakini ikifika mikononi mwa mteja ikawa ngumu kutumia. Kupitia majaribio haya, mjasiriamali hupata fursa ya kuboresha kabla ya uzinduzi rasmi na kuepuka hasara kubwa.

## Tatu: Jenga chapa

Bidhaa ikishaanza kuonekana, sasa ni wakati wa kuimarisha upande wa biashara na chapa. Panga bei na uwe na makadirio ya maingizo. Masuala ya kifedha ni muhimu ili kujua biashara itaishi kwa muda gani kabla ya kuhitaji mtaji zaidi.

Kwa upande wa chapa, ujumbe wako unatakiwa kueleza kwa uwazi kwa nini bidhaa yako ni muhimu kwa mteja. Ujumbe huu ulingane na jina la bidhaa, nembo, rangi, na mtindo wa mawasiliano. Hatua hii pia inahusisha kupanga mkakati wa uzinduzi, kama kampeni za kabla ya uzinduzi, ushirikiano na watu wenye ushawishi, au matukio ya kutambulisha bidhaa.

## Nne: Sambaza bidhaa sokoni

Baada ya maandalizi, sasa ni wakati wa kupeleka bidhaa sokoni. Unahitaji kuchagua njia sahihi ya mauzo, iwe ni kuuza moja kwa moja kwa wateja, kupitia majukwaa ya mtandaoni, au kushirikiana na maduka ya rejareja. Uchaguzi huu unategemea aina ya bidhaa na tabia za walengwa wako.

Wakati huo huo, usimamizi wa mnyororo wa ugavi ni muhimu sana. Kuanzia upatikanaji wa malighafi, uhifadhi wa bidhaa, vifungashio, ukaguzi wa ubora hadi usafirishaji, kila hatua ina mchango katika kuridhisha mteja. Uzinduzi pia unahitaji kuungwa mkono na matangazo, maudhui ya kuvutia, na mikakati ya uhusiano na vyombo vya habari ili kuongeza mwonekano wa bidhaa.

## Tano: Kuwa tayari kubadilika

Biashara yenye mafanikio ni ile inayojifunza na kubadilika. Baada ya bidhaa kuingia sokoni, kazi hajaishi. Ni muhimu kuendelea kuchambua maoni ya wateja, takwimu za mauzo, na matokeo ya kampeni za masoko. Taarifa hizi hukusaidia kubaini nini kinafanya kazi na nini kinahitaji kuboreshwa.

Wakati mwingine mjasiriamali hugundua kuwa hitaji la soko ni kubwa kuliko alivyotarajia. Hii inaweza kusababisha kupanua bidhaa au kuongeza aina mpya ili kuwafikia wateja wengi zaidi. Uwezo wa kubadilika ndiyo siri ya kudumu sokoni.